CHUO CHA BIBILIA

VITABU VYA

INJILI YA LUKA NA YOHANA

KITABU CHA KUMI NA MOJA

Sura Ya Kwanza

'Baadhi Ya Mitazamo Katika Injili Ya Luka'

Mwandishi wa Injili ya Luka hakuwa Myahudi wala mmoja wa mitume wale kumi na wawili. Yeye alikuwa Myunani na alielekeza Injili yake kwa Myunani. Wasomi wanaamini kwamba Luka alikuwa na Mariamu, mamake Yesu, Yakobo, nduguye Yesu pamoja na wengine walioshuhudia kuwa kina cha yake aliyoandika katika Injili hii ni kazi na maisha yake Yesu. Paulo alimtaja Luka kama kuwa 'tabibu mpendwa' na mwenziwe katika safari zao nyingi. Ni wazi kwamba alisafiri pamoja na Paulo hili kutibu udhaifu iliotokana na 'mwiba uliokuwa katika mwili' wa mtume huyu (2 Wakorintho 12). Paulo alimtaja Luka mara tatu katika nyaraka zake (Wakolosai 4:14; 2 Timotheo 4:11' Filemoni 24).

Pia, Luka ndiye mwandishi wa kitabu cha Matendo ya Mitume, ambacho kimeandikwa kwa mtu yule yule, Theofilo. Kwa kuwa jina hili pia maanake ni 'mpenda Mungu', baadhi ya wasomi huamini kwamba vitabu hivi viwili vimeandikiwa kwa kila mpenda Mungu, ilhali wengine wanaamini kwamba huyu Theofilo alifahamika sana na Luka.

Mwandishi wa Injili hii ni mtu aliyekuwa na elimu nzuri. Angetambulika kama mwana-sayansi siku hizi. Alitumia sana msemo wa matibabu kuliko *Hippocrates,* ambaye anatambulikana kama 'mkongwe wa utibabu siku hizi.' Pia, alitumia lugha sanifu ya Kiyunani katika Agano Jipya kuliko waandishi wale wengine, akiwemo Paulo. Alikuwa mwandishi mwenye ufasaha mwingi na mwana-historia aliyekuwa na usahihi mkuu.

Wakati Luka aliponakili safari za Paulo za umishionari, alitumia usemi wa 'sisi' na 'wale' kwa kupokezana. Uchuguzi wa vifungu hivi vya 'sisi' katika kitabu cha Matendo utatuonyesha wakati Luka alipoambatana na Paulo katika safari za umishionari. Paulo aliwaandikia Wakorintho kwamba, Mungu hawaiti watu wengi katika wokovu ambao ulimwengu unawatambua kama wenye maarifa (1 Wakorintho 1:26-29). Pamoja na Luka, walikuwa sio wa kawaida kwa ile kanuni ambayo inaweza kuwa ndio sababu yao kuwa na uhusiano wa karibu.

Luka ananakili miujiza ishirini, sita kati yake imenukuliwa tu katika Injili yake. Yeye ananakili hadithi za mafumbo ishirini na tatu, kumi na nane ambazo zinapatikana katika Injili yake.

Injili ya Luka inapendwa na watu wengi kwa kuwa Kristo anaelezwa kama mwenye utu wa kibinadamu, mwenye rehema nyingi, mwenye kuwajali watu na anayejitambulisha kikamilifu kwa utu wetu wa kibinadamu. Kama tabibu, Luka alikuwa na ufahamu mkuu wa kijamii. Anatupa historia ya maisha ya Kristo, ambaye alikuwa na ufahamu mkuu kuhusu wanadamu. Kila mara anapotilia mkazo hali ya utu wa mwanadamu, Luka anatuambia kwamba Martha alikasirika kwa kuwa Mariamu hakumsaidia katika maandalizi na utumishi, wakati Yesu alipokuwa mgeni wao kwa chakula cha jioni (10:38-42). Akiwa mwenye macho yenye umakinifu mkuu wa mwana-historia, na mwenye uzingatifu kwa yote yaliyomo pamoja na moyo wa huruma, Luke anatueleza kwamba macho ya Bwana yalikutana na yale ya Petro wakati jogoo alipowika; baada ya Petro kumkana mara tatu (22:60,61).

Kote katika Injili ya Luka tunaona utu wa kibinadamu wa Yesu. Unapounganisha yote, unapata picha na maelezo ya Yesu Kristo ambayo ni maelezo mengi juu ya Mwana wa Mungu na wa Adamu jinsi alivyokuwa, na yuko hata siku ya leo. Ujumbe wa Injili hii ya tatu ni utu wa Mungu-Mwanadamu. Mkazo ni kwamba huyu Mtu, ambaye ni Mungu, alijitambulisha kwa utu wa kibinadamu.

Na kama mwandishi sahihi wa historia aliye bora, anaandika ‘mambo kwa utaratibu’ kwa rafikiye Theofilo, ambaye naamini kwamba alikuwa mtu halisi, mwenye umuhimu mkuu mcha Mungu ambaye Luka alimpenda (1:3). Katika utangulizi wa kitabu hiki cha historia katika Agano Jipya, anaeleza Injili hii ya tatu kama nakala ya *‘yote ambayo Yesu alianza kutenda na kufundisha, hadi siku ile alipochukuliwa juu* (Matendo 1:1,2).’

Mwana-historia huyu anapasha zaidi kuhusu kuzaliwa na miaka thelathini ya kwanza ya maisha ya Yesu, kuliko mwandishi mwingine wa Injili. Sura za kwanza mbili zimetenga mistari mia moja na thelathini na mbili katika kuondolea mbali kimya. Injili ya Luka ni yenye utaratibu, na usanifu mkuu wa habari za kihistoria za mambo yale Yesu aliyotenda na kufunza tangu kuzaliwa hadi kupaa kwake mbinguni. Wasomi wengi wanaamini kwamba huu ndio msitari wenye maelezo halisi na muhimu katika Injili hii: *‘Kwa kuwa Mwana wa Adamu alikuja kutafuta na kuokoa kile kilichopotea* (Luka 19:10).’

Sura Ya Pili
'Dhana Ya Krismasi'

Kulingana na Luka, wakati Mungu alipokutana na historia ya mwanadamu na kutwaa utu wa mwanadamu, Aliwakaribisha watu fulani kushiriki katika muijiza Wake mkuu. Ingawa walikuwa wachache tu, kama mifano kwetu, kila mmoja wao ana kitu fulani cha kutufunza.

Bikira Mariamu

Malaika Gabrieli alimtembelea Mariamu, mwanamwali bikira ambaye alikuwa ameposwa na mtu aliyeitwa Yusufu. Gabrieli alimwambia Mariamu habari sawa na zile alizomwambia Zakaria - kuhani aliyekuwa babake Yohana Mbatizaji - kwamba Mungu angefanyika mwanadamu. Kuhani huyu hakumwamini Malaika na kwa sababu hiyo, Malaika akamwambia kwamba mdomo wake utafungwa naye hatakubaliwa kumwambia ye yote kuhusu muijiza huo mkuu ulipotimika. Malaika Gabrieli alikuwa amemwambia Mariamu kwamba angelichukua mimba na kumbeba Mwana wa Mungu. Naye Mariamu akamwuliza hivi, *'Litakuwaje neno hili, maana mimi sijui mume?* (1:34).'

Ingawa Mariamu alimwuliza Malaika maswali kuhusu vile bikira angemzaa mwana, yeye hakutilia shaka kama Zakaria. Kuhaki huyo ambaye hakuamini kwamba muijiza wa mwanawe ungewezekana, kwa kuwa mkewe alikuwa tasa wa umri mkuu. Mariamu hakuwa na shaka ila tu alishangaa vile Mungu angemwezesha bikira kuzaa. Kwa hakika, tunagundua kwamba Mariamu aliamini maneno ya Malaika wakati Elisabeti aliposema naye hivi: *'Heri aliyesadiki; kwa maana yatatimizwa aliyoambiwa na Bwana (*45).'

Imani Ya Wachungaji Wa Kondeni

Malaika waliwatokea baadhi ya wachungaji ambao walikuwa kondeni usiku wakichunga mifugo wao. Malaika waliwaletea Habari Njema za kuzaliwa kwake Kristo (2:10,11). Hebu tambua kwamba Habari Njema zilizotangazwa na Malaika zilikuwa kwa ajili ya kila mtu. Baada ya kupokea ujumbe huo - kabla na baada ya kuona huo muijiza - wale wachungaji walimwambia kila mtu yale Malaika waliyoyasema.

Je! Umewahi kushangaa ni kwa sababu gani Mungu aliwaambia wachungaji kuhusu muijiza huu wa Krismasi ya kwanza? Wale wengine ambao walielezwa kuhusu huu muijiza walikuwa na fursa muhimu sana na inaonekana kwamba Mungu aliwaambia kwa njia ya kuwafahamisha tu. Kuhani pamoja mkewe Elisabeti - wazazi wake Yohana Mbatizaji - walihitaji kufahamu. Mariamu na Yusufu walihitaji kufahamu na kuamini, licha ya kuwa tunasoma kwamba Mariamu *'akayaweka maneno hayo yote, akiyafikiri moyoni mwake* (2:19).'

Nao wachungaji kwa upande mwingine, walimwambia kila mtu yale ambayo walishuhudia na kusikia, kabla na baada ya ule muijiza mkuu. Ni kwa sababu gani Mungu aliwahusisha wachungaji katika muijiza huu mkuu? Ni kwa sababu alifahamu kwamba wangeamini na kuwaambia watu wengine habari za muijiza wa Mwokozi, ambaye ni Kristo - Masihi aliyeahidiwa na Bwana.

Yesu Mwenye Umri wa Miaka Kumi na Miwili katika Hekalu

Luka akivunja kimya na kutueleza jambo ambalo ni la kipekee kuhusu Yesu katika miaka yake thelathini aliyoishi ulimwenguni tangu kuzaliwa na kuanza huduma yake kwa watu. Hili ni tukio ambalo lilifanyika wakati alipokuwa na umri wa miaka kumi na miwili. Wazazi wake walimpeleka huko Yerusalemu wakiwa miongoni mwa maelfu ya watu waliokwenda kuandikwa.

Njiani wakirudi nyumbani, iliwachukua mwendo wa siku tatu kutambua kwamba Yesu hakuwa pamoja nao. Ndipo wakarudi kwa hofu hadi Yerusalemu na kumpata ndani ya Hekalu akiwauliza viongozi wa dini maswali. Wakati wazazi wake walipoeleza hofu zao katika kumtafuta, Yeye awajibu hivi*: 'Kwani kunitafuta? Hamkujua ya kuwa imenipasa kuwamo katika nyumba ya Baba yangu?* (2:49).'

Jambo hili linawafanya wazazi wake kuonekana kuwa wanadamu wa kawaida - kwa kumpoteza mwana na baadaye kumpata mahali ambapo hawakumtarajia hata kidogo. Kisha kusikia kutoka kwake kwamba iliwapasa wao kutambua kwamba Yeye angelikuwa katika kazi ya Baba yake, Hekaluni, pale ambapo walimpata akiwauliza maswali waandishi, wasomi wakuu na waalimu. Hii ilifanya tukio hili kuwa la kutambuliwa sana.

Matumizi Ya Kibinafsi

Agano la Kale na Jipya zinatuambia kwamba Yesu atakutana na historia ya wanadamu kwa mara nyingine katika muijiza wa kuja kwa mara ya pili. Hali halisi ya Krismasi ya kwanza ni

kwamba Mungu alifanyika kuwa mwili wa mwanadamu kwa ajili ya wokovu wetu. Ilhali hali halisi ya mjio wa pili wa Kristo ni sawa na huo. Kwa maelezo mengine, Mungu atafanya Krismasi nyingine – kuna Krismasi nyingine inayokuja. Sawa na Krismasi ya kwanza ilivyokuwa tumaini la kipekee tulilokuwa nalo kwa wokovu, mjio wa pili ni tumaini la pekee la Kanisa

Mungu ametupa maarifa ya baraka na tumaini la kipekee kupitia Neno Lake. Yeye anataka kutumia sisi hili kutangaza Habari Njema ya kurudi kwa Mwanawe katika ulimwengu ambao umejawa watu ambao hawana tumaini. Ikiwa kama Zekaria, twatilia shaka muijiza huu, kutokuamini kwetu kutatufanya bubu nasi hatutashiriki tumaini hili na mtu ye yote. Ikiwa kama Mariamu tutauliza maswali na kuchuguza mambo yote ya mjio wake, yamkini kwamba tutafikiria mambo mioyoni mwetu bali hatutawaeleza wasio na matumaini kuhusu tumaini lao la pekee.

Ni lazima tufuate mfano wao wale wachungaji na kuwaambia watu wote Habari hizi Njema kabla yao kuaona kwanza. Je! Utaufuata mfano wa wachungaji na kuwaambia watu unaowajua kuhusu tumaini lenye baraka ulio nalo kama mwaminifu ambalo kwa uhakika ni la kipekee kwa ulimwengu huu?

Sura Ya Tatu
‘Maongozi Au Sera Ya Masihi’

Kwa hakika kuna vifungu viwili vinavyofungua ufahamu wetu wa Injili ya Luka. Tayari nimekitaja cha kwanza (Luka 19:10). Yesu anatupa kifungu cha pili wakati anapoenda katika Sinagogi huko mjini Nazareti na kusoma chuo cha nabii Isaya (Luka 4:18). Ikiwa utalinganisha vifungu hivi viwili, utaona kwamba kwa ufasaha mkuu, vinatangaza kusudi ambalo lilimleta Yesu.

Ukitazama katika hali yake, msitari wa kwanza ni picha ya Mwokozi wa ulimwengu, jinsi alivyokuwa wakati mwingi - akiwatafuta na kuwaokoa waliopotea (Luke 19:10). Hata hivyo, wakati fungu lile lingine linapotazamwa katika hali yake, linatumika kama: ‘maongozi au sera ya Masihi (Luka 4:18).’ Maongozi ni tangazo kamili kutoka kwa Yesu kwa juu ya sababu yake kuja

na kile alichokuwa akitenda. Wakati mwingine yanatajwa kama ‘maongozi ya Nazareti,’ kwa sababu yalitangazwa katika mji wake hapo mwanzoni mwa huduma yake kwa watu.

Maongozi Yatangazwa

‘Akaenda Nazareti, hapo alipolelewa; na siku ya Sabato akaingia katika Sinagogi kama ilivyokuwa desturi yake, akasimama ili asome. Akapewa chuo cha nabii Isaya, akakifungua chuo, akatafuta mahali palioandikwa, Roho wa Bwana yu juu yangu, Kwa maana amenitia mafuta kuwahubiri maskini habari njema. Amenituma kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao, Na vipofu kupata kuona tena, Kuwaacha huru waliosetwa . . .

Akakifunga chuo, akamrudishia mtumishi, akaketi; na watu wote waliokuwamo katika Sinagogi wakamkazia macho. Akaanza kwa kuwaambia, Leo Maandiko haya yametimia masikioni mwenu (Luka 4:16-21).’

Viongozi wengi ulimwenguni wameanza harakati za kuandika sera za uongozi wao ambazo ni tangazo la jawabu na suluhisho ambazo wao husema kuwa wako nazo kwa matatizo ya watu katika ulimwengu huu. Wakati tunaposikia kwamba Yesu alianza huduma yake ya miaka mitatu kwa kuitangaza sera yake ya Nazareti, twahitajika kutambua kwamba tunasikiza sera kuu ya uongozi ambayo tumewahi kusikia kwa kuwa ilitimizwa kikamilifu na Yeye aliyeitangaza.

Twahitajika pia kutambua kwamba Yesu alikuwa akitangaza sera ya uongozi wa Kanisa la siku ya leo kwa njia ambayo Luka anatuambia kuhusu vile huduma Yake ilivyoanza. Sera ya uongozi ya Nazareti haituonyeshi tu kile Yesu alichokuwa akitenda alipokuwa ulimwenguni kwa hali ya mwili, bali pia inatuonyesha kile anachotaka kutenda kupitia wale tunaojiita ‘Mwili wa Kristo.’

Kundi moja la kiulimwengu lilikuwa kwa wakati mmoja na wafuasi wachache sana hata baada ya kuchapisha sera ya uongozi wake. Kisha mfuasi mmoja akaandika kijikaratasi kidogo kilichokuwa na maandishi, ‘Ni kipi kinahitaji kutendwa?’ Ushawishi mkuu wa kijikaratasi hiki ulikuwa, ‘ni kipi ambacho chahitajika kutendwa na wale wanaoamini sera ya uongozi?’ Kijikaratasi hicho kimewanufaisha mamilioni ya watu katika kundi hilo sasa.

Maisha pamoja na mafundisho ya Yesu Kristo ndio Sera ya uwanafunzi Wake. Wafuasi wa kweli wa Yesu Kristo huamini kwamba Kristo aliyefufuka, ambaye yu hai ana suluhisho la pekee kwa mahitaji na matatizo ya watu wa ulimwengu huu. Tangazo hili la Yesu hapo mwanzoni wa huduma Yake ni furushi dogo la Sera uongozi ambayo bali na kutuonyesha yale tunayopaswa kutenda. Ujumbe huu wa huduma yake unatuambia yale yanayopaswa kutendwa na kila mwanafunzi Wake ulimwenguni huu wa leo.

Muhutarsari huu wa tangazo la malengo ya huduma ya Yesu unatuonyesha uchuguzi mfupi wa Injili ya Luka. Tunapokagua Injili hii ya tatu pamoja, nitakuonyesha jinsi Yesu alivyotangaza sera ya uongozi wakati aliposoma kutoka kwa chuo cha Isaya huko Nazareti, kisha kuthibitisha kwa viongozi wa kidini wa siku zake kwamba Yeye alikuwa na mamlaka ya kutekeleza matakwa ya sera ya uongozi Wake. Injili ya Luka inaendelea kutuonyesha jinsi Yesu alivyotekeleza sera ya uongozi ambayo alitangaza na kuthibitisha. Mwishowe, nitakuonyesha vile Luka anaelezea Yesu akiwakaribisha na kuwapa changa moto wengine (yaani wewe na mimi), hili tufanyike washiriki pamoja naye katika utekelezaji wa sera ya uongozi Wake pamoja na huduma kuu hapa ulimwenguni.

Jinsi Luka anavyowasilisha maelezo ya historia ya maisha ya Yesu, inatupa ufafanuzi muhimu mwingine wa maanake kuwa mwanafunzi wa Yesu Kristo. anatuonyesha kile kinachohitajika kutendwa na Kanisa la Yesu Kristo katika ulimwengu wa leo.

Wakati mwingi mimi nimekuwa na wazo kwamba litakuwa bora, ikiwa mwanafunzi wa Yesu anaweza kusoma sera hii uongozi Wake kisha kuandika kijikaratasi kinachoitwa: 'Ni kipi kinachohitajika kutendwa na mwanafunzi mwaminifu wa sera ya uongozi wa Yesu?' Mwishowe, nilitambua kwamba hakuna mwanafunzi ambaye anaweza kuandika kijikaratasi kile kwa kila mmoja wetu. Hii ni kwa sababu Mungu amepanga mapenzi na ufunuo wa mapenzi Yake kwa maisha ya kila mmoja wetu kwa njia ambayo ni lazima tuje mbele zake jinsi Paulo alivyomwendea katika njia ya kwenda Dameski, na kuomba, *'Bwana, wataka mimi nitende nini?* (Matendo 9:6).'

Maongozi Ya Masihi Yathibitishwa

Yesu alikuwa akiponyana na kufunza katika nyumba huko Karpenaumu. Viongozi wa dini ambao walifahamika kama 'wataalamu wa sheria,' walikuwa wamesafiri kutoka kila pande za nchi ya Isareli, kutoka Yerusalemu hadi Galilaya, hili kuchuguza muijiza uliothibitika ambao

Yesu alikuwa amemponya mwenye ukoma. Hii inawasilisha mazingira ambayo Yesu anathibithsha Sera ya Uongozi ambayo alikuwa ameitangaza huko Nazareti. Anafanya muijiza mwingine kwa hali hii *'Ili mpate kujua ya kwamba Mwana wa Adamu anayo amri duniani ya kusamehe dhambi!* (Luka 5:17-26).'

Hali Yesu akiendelea kufunza, watu wanne walitoa matofali juu ya dari na kwa kutumia kamba, walimshusha mwenzao ambaye alikuwa amepooza akiwa juu ya kitanda na kumweka mbele ya Yesu. Yesu hakuwa na pingamizi bali fursa pekee. Alitumia fursa hii hili kuthibitisha Sera ya Uongozi wakati alipomwambia yule mtu aliyekuwa mbele zake, 'Dhambi zako zimesamehewa!' Wale viongozi wa dini mashuhuri walishangazwa na hata kuuliza, '*ni nani awezaye kusamehe dhambi isipokuwa Mungu peke yake?'*

Aliwajibu kwa swali hili: '*Lililo jepesi ni lipi? Kusema, Umesamehewa dhambi zako, au kusema, Ondoka, uende? Lakini mpate kujua ya kwamba Mwana wa Adamu anayo amri duniani ya kusamehe dhambi,* (alimwambia yule mwenye kupooza*) Nakuambia, Ondoka, ujitwike kitanda chako, ukaende zako nyumbani kwako. Mara hiyo akasimama mbele yao, akajitwika kile alichokilalia, akaenda zake nyumbani kwake, huku akimtukuza Mungu* (5:23-25).'

Wakati Yesu alipomwambia mtu huyo kuwa dhambi zake zimesamehewa, hawa wakuu hao wa dini waliwazia haya, 'sisi tunalo tu Neno Lako peke yake kwa ushahidi huu!' Yeye alikubaliana na wana theolojia hao kwamba ni Mungu peke Yake anayesamehe dhambi. Kupitia muijiza huu, Yeye alithibitisha kwamba alikuwa Mungu pamoja nasi na kwamba alikuwa na mamlaka sawa ya kusamehe dhambi humu duniani kama vile Mungu alivyo huko mbinguni. Hivyo basi, Yeye alithibitisha kwamba alikuwa na uwezo na mamlaka ya kutekeleza matakwa na masharti ya Sera ya Uongozi Wake.

Utekelezaji Wa Sera Ya Nazareti

Yesu alitangaza kwamba Roho wa Mungu alikuwa amempaka mafuta kwa kusudi. *'Kwa maana amenitia mafuta kuwahubiri maskini habari njema.'* Yeye hakuwa tu akigusia kuhusu wale walio maskini kiuchumi katika kifungu hiki, bali pia kwa wale waliokuwa maskini wa kiroho; wale ambao hawajawahi kusikia Habari Njema ya wokovu. Wao walikuwa maskini kwa hali kuwa walikuwa vipofu, wenye kufungwa na wenye mioyo iliyovunjika.

Maskini vipofu walikuwa ni wale ambao hawakufahamu mbele wala nyuma, na kwamba walikuwa wametawanyika kama kondoo wasio na mchungaji (Mathayo 9:36). Walikuwa vipofu kiroho. Lengo kuu la huduma yake lilikuwa kuihubiri Injili, kufunza kwa nia kwamba hawa vipofu wa kiroho wangeweza kuona. Aalitumia mafunzo Yake katika mijadala yake, hadithi za mafumbo, mahojiano pamoja na matendo ya kuleta kuona kwa vipofu wa kiroho.

Yesu pia alitangaza Habari Njema Yake kwa wale waliokuwa wamefungwa. Alitumwa hili 'kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao,' na kwa maelezo mengine, kuwaweka huru waliofungwa (Luka 4:18). Unaweza kuona kwamba katika Injili zote, Yeye hangeweza kumpata mtu aliyekuwa amefungwa na kumwacha kwa kile alichotaja kama kufungwa. Hali hii ya kushangaza inadhihirishwa vyema zaidi katika hali ya yule mwanamke aliyekuwa amefungwa na Ibilisi kwa miaka kumi na nane na kufanywa huru na Yesu (Luka 13:16). Yeye alifafanua zaidi lengo hili kuu la huduma Yake katika mazungumzo makali ambayo alihusika na wale viongozi wa dini (Yohana 5:8:30-35).

Yesu alieleza mambo magumu maishani kuwa kama dhoruba au tufani. Alitangaza kwamba dhoruba huja katika maisha ya kila mmoja wetu. Wakati zile dhoruba zinapowapiga watu chini, wengi huyumbayumba, ilhali wengine huangamia kabisa. Wakati Isaya na Yesu wanapoeleza kuhusu watu wenye kutoneshwa au kujeruhiwa na mioyo iliyovunjika, hawa ni watu ambao wameangamizwa na dhoruba zao. Huruma ya Yesu kwa watu hawa wenye kuvunjika ni jambo lenye kugusa moyo katika huduma na maisha Yake. Na kama tabibu mwenye huruma nyingi, Luka anatilia mkazo dhamira yake ya kijamii na rehema ya Yesu kwa watu waliovunjika katika ulimwengu huu.

Je! Wewe ni kipofu wa roho? Je! Wewe wajihisi kuwa mpotevu hivi kwamba haufahamu pahali pa kupindukia? Je! Wewe uko huru? Je! Wewe unafanya kile unachopenda kufanya au kile ambacho ni lazima utende? Je! Wewe ni mfungwa wa dhambi au tabia kiasi kwamba huwezi kutenda jambo lingine isipokuwa mambo yanakuogoza kwayo? Je! Wewe umevunjika na kujehuriwa au kutoneshwa, na huwezi kupata uponyanji kutokana na kuvunjika kwako?

Ikiwa majibu yako kwa mojawapo ya maswali haya au yote kati ya maswali haya ni ya kukubalika, basi Luka anaeleza hadithi hii ya maisha ya Yesu kwa njia ambayo inaonyesha na

kutufahamisha kwamba sisi ni watu halisi ambao ndio sababu ya Yesu Kristo kuja ulimwenguni. Alikuja hili tupate kuona tena kutokana na upofu wetu, kutufanya huru kutokana na utumwa na kuleta uponyaji kwa kuvunjika kwetu. Azimia kumwamini na kumpokea Kristo ambaye unakutana naye katika Injili ya Luka. Jitolee kumfuata kama mwanafunzi wake naye atakufanya kuwa mzima kwa njia zote.

Sura Ya Nne
'Ushirikiano Wa Maongozi'

Jambo la mwisho ambalo tunaweza kuona kuhusu jinsi sera ya uongozi inavyoonyesha mfumo wa Injili hii ya Luka ni utambulizi kwamba wakati wote, Yesu alikuwa akifundisha na kuwafanyiza mitume wake kazi sawa na kuwapa changa moto kufanyika washiriki wake katika utekelezaji wa lengo kuu la huduma Yake jinsi alivyotangaza huko Nazareti. Mfano wa kwanza ulio dhahiri ni vile alivyomwandikisha Petro kuwa mshiriki pamoja naye katika utekelezaji wa sera hiyo ya uongozi.

Asubuhi moja na mapema katika ufuo wa bahari ya Galilaya, hali Yesu akifunza kundi kuu la watu, Alimwuliza Petro, ambaye alikuwa amechoka baada ya usiku kucha bila mafanikio katika uvuvi, kama angetumia mtumbwi wake kama mimbara ya kuhubiria. Yaonekana kwamba Yesu alikuwa akihitaji pahali palipokuwa pameinuka hili aweze kuwasiliana vyema na kundi hilo kubwa la watu ambalo lilikuwa limemsonga hadi ukingoni mwa ziwa (Luka 5:1-11).

Hii haikiwa mara ya kwanza ya Yesu kukutana na Petro. Hii ilitendeka wakati nduguye Petro kwa jina Andrea alipomtambulisha kwake (Yohana 1:41,42). Tunajulishwa kwamba Yesu alifanya mwaliko kwa hawa ndugu, pamoja na washiriki wenzio katika biashara ya uvuvi, yaani Yakobo na Yohana, ambao walikuwa pia ndugu. Mwaliko huu ulikuwa, '*nifuateni Mimi nami nitawafanya kuwa wavuvi wa watu* (Mathayo 4:19).' Haya ndio maelezo mapana ya Luka kwa yale Mathayo anayotaja katika msitari mmoja. Au inawezekana kuwa Luka anatuambia kwamba Yesu anarudia na kutilia mkazo mwito wake kuonyesha kile Petro anachohitaji kufunza ikiwa atakuwa mvua watu.

Baada ya wakati wa kujifunza, Alimwambia Petro hivi, ‘ningependa kama ungenichukua kwenda kwenye uvuvi!’ Alimpa changa moto Petro kuchukuwa mtumbwi wake hadi penye maji mengi. Kisha akamshauri kutupa nyavu zake majini na kuvua samaki wengi! (4).

Huku Yesu akiendelea kufunza watu hao, tunasoma kwamba Petro alikuwa akiosha nyavu zake baada ya usiku kucha baharini bila kuvua cho chote. Naweza kumwona Petro akiwa mwenye hamaki kwa sababu hakufanikiwa katika uvuvi asubuhi hiyo. Pia, naweza kumwona Yesu akiendelea kufundisha watu, akiwa mwenye huzuni nyingi kwa huyu mvuvi kuliko kundi hilo.

Yesu alijua kuwa kwa muda wa miaka mitatu, huyu mtu, ambaye hangeweza kuwavua samaki, angehubiri ujumbe siku ya Pentekoste ambao ungesababisha wokovu kwa watu elfu tatu, huku maelfu wengine wakiokolewa kila mara anapohubiri Injili siku za Pentekoste zilizofuata (Matendo 2:14-42).

Pia, alifahamu kwamba miaka mitatu tangu asubuhi hiyo, wakati kivuli cha mvuvi huyu kitawaangukia watu waliokuwa viwete wasio na matumaini, nao wangeponywa kwa njia ya mwujiza! (Matendo 5:12-16). Hii ndio sababu naamini kwamba Alikuwa akihusika zaidi na Petro siku hiyo kuliko makutano makubwa.

Je! Yesu angebadilisha mtu huyu kwa njia gani, ambaye hangeeza hata kuvua samaki, kuwa mtu ambaye pamoja na Paulo, wangekuwa wavuvi wakuu wa watu ambao ulimwengu umewahi kushuhudia? Nguvu za kiroho ambazo zajibu maswali yangu zatukia katika mapatano ya Yesu na Petro. Yesu ampa Petro changa moto kuwa na mapatano ya ushirika pamoja naye katika utekelezaji wa lengo kuu la huduma jinsi ilivyotangazwa katika Sera ya Nazareti.

Wakati Yesu na Petro walipokuwa mahali penye maji mengi, Yesu alimwambia ashushe nyavu yake kwenye maji. Petro akajibu kwa kusema*, ‘Bwana mkubwa, tumefanya kazi ya kuchosha usiku kucha tusipate kitu. . .’* Kwa mara nyingine, mimi nafikiri kuwa, kulikuwepo na muda mfupi wa kimya kabla ya kujibu kwake Petro wakati macho ya Yesu na Petro yalipokutana kisha Petro akaendelea kusema*, ‘Lakini kwa neno lako nitazishusha nyavu* (5).’

Wakati zile nyavu zilipovutwa juu, zilikuwa zimejaa samaki wengi! (6-7). Kwa mshangao wake kwa ajili ya mwuijiza mkuu, Petro alianguka magotini pa Yesu, akisema, *'Ondoka kwangu, kwa kuwa mimi ni mtu mwenye dhambi, Bwana* (8).' *Naye Yesu akamjibu, 'Simoni, Usiogope, tangu sasa utakuwa ukivua watu* (10).'

Kabla ya kukutana na Yesu, maisha ya Petro yalikuwa na shauku kuu ambalo lilikuwa kuvua samaki. Maneno haya mawili ambayo Yesu alimwambia Petro yananivutia sana na ndio msemo mwingine wa Agizo Kuu: 'Kuvua watu!' Wengi Kanisani wana tabia ya kuwashuhudia wanawake pamoja na watoto kwa kuwa wao ni wepesi. Lakini, Yesu alifahamu kwamba wanawake na watoto huwafuata wanaume, hivyo basi ikiwa tutawavua wanaume, tutaifikia jamii nzima kwa ajili Yake.

Ni kwa sababu gani alipigwa na butwaa kwa mwuijiza wa kuvua samaki wengi hivi kwamba akajitaja kama mwenye dhambi, hata kumwambia Bwana amwondokee mbali? Baadhi ya wasomi husema kwamba Kristo alikuwa akihubiri kwa makutano kuhusu dhambi za binadamu, na kwamba Petro alikuwa akishuhudia hukumu ya dhambi, huku huu ukiwa wokovu wake.

Wasomi wengine wanaamini kwamba Yesu alikuwa akimsajili Petro kuwa na ushirika naye hili kumsaidia kutekeleza sera ya uongozi Wake. Inawezekana kwamba Petro alikuwa ametambua kwamba Kristo alikuwa akimwuliza hivi, *'Je! Utashirikiana nami katika kuwapa kuona wale walio vipofu na kuwaweka huru waliofungwa pamoja na kuwaponya waliovunjika? Utabadilisha thamani zako kutoka kuvua samaki hadi kuvua watu?'* Wasomi hawa wanaamini kwamba Petro alikuwa chini ya ushawishi wa hukumu kuu kwamba hakustahili mwito huo.

Inawezekana kuwa alikuwa akisema hivi*, 'Bwana, una mtu asiyestahili. Na haiwezekani kabisa kwako kuniita hili niwavue watu, kwa kuwa sistahili wala sijahitimu kabisa!'* Ikiwa hiki ndicho kina cha yale Petro aliyokuwa akinena, kwa hakika alikuwa akidhihirisha baraka za kwanza ambazo Yesu alikuwa ametoa mwongozo kwa kila mwanafunzi wake*: 'Heri walio maskini wa roho* (Mathayo 5:3).'

Hili kumbadilisha kabisa Petro kutoka mvuvi wa samaki ambaye hakuwa na fanaka ye yote hadi mvuvi wa watu aliyefanikiwa, ilimbidi Yesu kwanza kumfunza Petro ni nani aliyekuwa mvuvi kwanza katika ule mtumbwi wake siku ile. Wakati Petro alipoitana, 'Mwalimu,' alikuwa

akigusia jambo kwamba Yesu alikuwa Mwalimu, na kwamba mwenyewe, alikuwa mvuvi wa samaki. Kisha anaendelea kumshauri Bwana kuhusu jinsi ya uvuvi – 'Kila mvuvi wa samaki anafahamu kwamba ikiwa haukufanikiwa usiku, kwa hakika itakuwa vigumu sana kuvua samaki mchana' - Hii inatokea kuwa kina cha upinzani wake Petro.

Jambo la pili ni kuwa, ilimbidi Yesu kumfunza Petro kwamba hangeweza kuwavua watu hadi atakapofahamu kwamba, Kristo anayefufuka aliye hai, ndiye Mvuvi wa kweli wa wanadamu. Safari hizi mbili za Petro kwenda kuvua - moja ikiwa haikufanikiwa hata kidogo ilhali nyingine ikiwa imefaulu kwa njia isiyo ya kawaida, - ilimshawishi Petro kwa maisha yake yote kuhusu siri fulani za kiroho:

'Kuvua watu hakujalishi wewe ni nani ila Yeye ni nani. Kuvua watu kwa ajili ya Yesu hakujalishi wewe waweza kutenda mambo yapi, ila Yeye anaweza kutenda. Hili kuhusika kama mvuvi wa watu hakujumuishi kile ninachotaka bali kile anachotaka. Na wakati ambapo kuna uvuvi wa muijiza katika kuwavua watu, ni lazima wakati wote nikumbuke kwamba huo muijiza wa wokovu wa watu haukutokea kwa kuwa kuna jambo ambalo nilitenda ila kwamba ni muijiza usio wa kawaida ambao Yeye alitenda kupitia mwili wangu dhaifu na wenye mauti.'

Je! Unaona kwa nini Kristo analiyefufuka, aliye hai alimchagua Petro kuhubiri ujumbe siku ya Pentekoste na jumbe nyingine baada ya siku hiyo ambazo ziliwaongoza wengi kupokea wokovu? Ilikuwa kwa sababu Petro alikuwa amejifunza siri za kiroho kuliko mtume mwingine. Katika siku ya Pentekoste, wakati miujiza yote, pamoja na ishara na maajabu zilipokuwa zikifanyika, Petro alitangaza kwamba Kristo ndiye aliyehusika na miujiza hiyo iliyokuwa ikifanyika siku hiyo (Matendo 2:32,33).

Na Kristo, Ndani Ya Kristo Na Kwa Kristo

Baada ya tukio hili, tunasoma kwamba Petro pamoja na washiriki katika biashara yake '*waliacha vyote wakamfuata* (11). Sura hii katika safari ya kiroho ya Petro inatuonyesha daraja kadhaa za uhusiano katika safari yetu na Kristo. Daraja ya kwanza ni kuishi na Kristo - maanake ikiwa kupokea na kubarikiwa kwa wingi na njia zote ambazo Yeye hutuokoa kwa utukufu pamoja na kuokoa maisha yetu. Petro alipokea ujuzi wa kiwango cha kwanza cha uhusiano na Kristo wakati alipobarikiwa na ule uvuvi usio wa kawaida wa samaki wengi.

Kiwango cha pili cha uhusiano na Kristo ni wakati tunapoingia katika mipango Yake kwa maisha yetu, na kutupilia mbali mipango yetu wenyewe. Je! Umewahi kusikia watu wakisema hivi, 'Nimeamua kumchukua Yesu Kristo katika mipango yangu?' Hili linaweza kusikika kama jambo la muhimu kwa mara ya kwanza, lakini ukilitia maanani, sio kwetu kumkaribisha Yesu katika mipango yetu. Ni Yeye ambaye anataka kutukaribisha katika mipango Yake.

Kuna msemo katika Agano Jipya ambao unapendwa sana na mitume wakati wanapoelezea hatua ya pili katika uhusiano na Kristo. Usemi huu ni wa maneno matatu tu: 'Ndani ya Kristo.' Yesu anaeleza hatua hii ya uhusiano kwa fumbo lenye kuvutia mno. Kulingana na Yesu, twahitajika kuwa katika uhusiano pamoja Naye jinsi tawi linavyoshikamana na mzabibu (Yohana 15:1-16). Matunda huzaliwa kwa wingi katika tawi kwenye fumbo hili la Yesu. Hii inatufunza kwamba maneno haya matatu, 'ndani ya Kristo,' yanamaanisha kuwa ni chombo cha binadamu ambacho kazi yake Kristo inafanyika katika ulimwengu huu kwa kuwa tuko vyema 'ndani ya' - na kushikamana naye Kristo anayeishi.

Hatua ya tatu ya uhusiano na Kristo ni kuishi kwa Kristo (11). Hatua hii ya uhusiano inatilia mkazo nia na hamu tuliyo nayo katika kumfuata na kumtumikia Kristo anapohuzisha katika mipango yake ya kuufikia ulimwengu wetu kwa Injili Yake ya wokovu. Katika hatua hii ya uhusiano, huwa tunafanyika washiriki pamoja na Kristo anapowapa kuona wenye upofu, kuwafanya huru waliofungwa, kuwaponya waliovunjika mioyo na wale wenye jeraha katika ulimwenguni huu. Na Kristo, Ndani ya Kristo na kwa Kristo, sisi tu washiriki wake huku anapotekeleza lengo la huduma Yake aliyotangaza katika Sera ya Uongozi ya Nazareti. Katika hii hadithi yenye kuvutia, Petro aipitia mifano ya hatua tatu za uhusiano naye Kristo.

Je! Wewe umebarikiwa Na Kristo? Na Je! Wewe u Ndani ya Kristo? Je! Wewe unazaa matunda? Je! Unaishi kwa ajili yako mwenyewe au Kwa Kristo?

Sura Ya Tano
Mafumbo Ya Ushirika'

Unaposoma sura ya kumi na tano ya Injili ya Luka, utatambua kwamba unasoma moja wapo ya mafumbo makuu ambayo Yesu aliwahi kufunza. Kina cha fumbo hili ni ukweli ulio sawa tuliouona katika sura hii katika safari ya kiroho ya Petro. Yesu anawateua washiriki

ambao wataitenda kazi pamoja Naye huku akitimiza malengo yake ya huduma katika ulimwengu huu. Sura ya kumi na nne ilimalizika huku Yesu akihubiri moja wapo ya ujumbe wake wenye uzito sana ambao unafahamika kama usemi mgumu wa Yesu. Katika ujumbe huo, Yesu aliuliza kujitolea kikamilifu kwa wale ambao wangetaka kufanyika wanafunzi wake.

Fumbo La Vitu Vilivyopotea

Sura hii ya kumi na tano inaanza kwa kutuambia kuwa kulikuwa na mapokezi ya aina mbili kwa jumbe hizi zenye nguvu. Watoza ushuru na wenye dhambi walipokea vyema ujumbe huu. Wao walisongelea karibu na Yesu na kufanya duara la ukaribu. Lakini Mafarisayo na Waandishi walijiondoa karibu na Yesu yamkini hatua ishirini na kufanya duara lingine la nje. Yesu alitangaza kile kinachoweza kutajwa kama fumbo kuu zaidi kwa makundi hayo mawili ya duara yaliyomzunguka na aina mbili tofauti za watu: karibu na Yesu, kulikuwa na duara la wenye dhambi na watoza ushuru ambao walikuwa wakiokolewa. Kisha kulikuwepo na duara lingine kubwa lililomzunguka, la watu wa kidini ambalo lilisongea mbali na kuuliza*, 'Mbona yeye anahusika na wenye dhambi na watoza ushuru?'*

Funzo hili kuu la Yesu sio kama vile watu wengine walifikiria kuwa mfululizo wa hadithi zenye mafumbo, bali ni 'fumbo la vitu vilivyopotea,' lenye kuendelea. Fumbo hili linaelekezwa kwa duara la nje, likiwafafanulia kile kilichokuwa kikiendelea katika duara la ndani. Kwa hali hii, Yesu pia anawasihi walio katika duara la nje kushirikiana naye katika kile kilichokuwa kikiendelea kwenye duara la ndani.

Yesu anaanza na fumbo hili kwa njia hii: '*ni nani kati kwenu, mwenye kondoo mia, akipotewa na mmojawapo, asiyewaacha wale tisini na kende nyikani, aende akamtafute yule aliyepotea hata amwone? Naye akiiisha kumwona, humweka mabegani pake akifuhari. Na afikapo nyumbani kwake, huwaita fariki zake na jirani zake, akawaambi, Furahini pamoja nami, kwa kuwa nimekwisha kumpata kondoo wangu aliyepotea. Vivyo hivyo kutakuwa na furaha mbinguni kwa ajili ya mwenye dhambi mmoja atubuye, kuliko kwa ajili ya wenye haki tisini na kenda ambao hawana haja kutubu.'*

Yesu anawaambia wale walioko katika duara la nje: 'ninyi mwaitazama duara iliyo ndani, na kile ambacho mnaona ni watoza ushuru na wenye dhambi, makahaba, na wezi na watu waliopotoka. Lakini hebu niwaambie kile ambacho Mungu anachokiona. Mungu anawaona hawa watu kama kondoo waliopotea. Wakati wote kondoo aliyepotea

anapopatikana, kuna furaha kuu mbinguni.' Yesu alikuwa akiwapa changa moto wale waliokuwa katika la duara la nje kwa njia hii: 'Mungu anawathamini sana wenye dhambi waliopotea. Mbona ninyi hamna furaha wakati hawa kondoo waliopotea wanapopatikana?'

Kisha baadaye, Yesu akawaambia hadithi kuhusu sarafu iliyopotea. Alisema, 'au kuna mwanamke gani mwenye shilingi kumi naye akipotewa na moja, asiyewasha taa na kufagia nyumba, na kutafuta kwa bidii hata aione? Na akiisha kuiona, huwaita rafiki zake na jirani zake, akawaambia, Furahini pamoja nami, kwa kuwa nimeipata tena shilingi ile iliyonipotea.!'Kuna tafsiri kadha ambazo zaweza kutumika katika sehemu hii ya fumbo. Lakini funzo kuu ni kwamba, shilingi ile ya mwanamke, ilikuwa imempotea na baadaye ikapatikana tena.

Mimi nilipoteza sarafu yenye thamani kuu nilipokuwa ningali mchanga. Ilitumbukia kwenye shimo la mfereji wa kupitishia maji machafu, ambapo palikuwa na kizuizi cha chuma yenye fito. Sarafu hiyo ilitumbukia ndani umbali wa futi moja u nusu lakini singeweza kulifikia kwa kuwa zile fito zilikaribiana mno hivi kwamba vidole vyangu vidogo havingeweza kuingia mle. Nilifedheheshwa mno.

Mkongwe mmoja alikuwa akipita pale naye akajitolea kunisaidia. Alichukua gundi niliyokuwa nikitafuna na kuiweka kwenye ncha ya mwavuli wake. Kisha akauingiza katika shimo lile na kuigusa lile sarafu kisha akaivuta nje na kunipatia. Sarafu hilo lilikuwa na thamani mara mbili, kwa kuwa nilikuwa nimeipoteza na sasa nimeipata tena.

'Kukomboa' humaanisha 'kununua tena' na 'kurudisha tena' kile kilichokuwa kimepotea. Sisi tu wenye thamani kuu zaidi kwa Bwana kwa kuwa tu kama ile sarafu iliyopotea wakati anapotupata kupitia ukombozi uliowezekana kufuatia kifo na ufufuo wa Mwanawe.

Hii ndio maana halisi ya dhana kuhusu ukombozi na sarafu iliyopotea kisha kupatikana tena katika fumbo la Yesu. Kwa hahika, hili ni fumbo dhahiri kuhusu ukombozi ambao unafundishwa kote katika Biblia kwa vile vitabu vya Kutoka, Kumbukumbu la Torati, Ruthu, pamoja na Mitume katika Maandiko yaliyomo katika Agano Jipya (1 Petro 1:18, 19). Ni wazi kwamba Yesu anazungumza na duara la nje, '*Hawa watu wamepotea lakini wao wakombolewa. Nao malaika wote mbinguni wafurahia! Mbona ninyi hamfurahii?'*

Kisha Yesu akasema, *'Mtu mmoja alikuwa na wana wawili. Yule mdogo akamwambia babake, Baba, nipe sehemu ya mali inayoniangukia. Akawagawia vitu vyake. Hata baada ya siku si nyingi, yule mdogo akakusanya vyote, akasafiri kwenda nchi ya mbali; akatapanya.'* Hii ni hadithi inayofahamika sana ya mwana mpotevu. Duara hizi mbili ni hali ambayo Yesu anazitumia katika kuieleza hadithi hiyo. Yeye anawaeleza walio katika duara la nje, yale yanayotendeka katika duara la ndani; kile kinachotendeka wakati anapotoa hadithi ya mwana mpotevu. Yesu anawaambia wale Mafarisayo wenye chuki kuwa, 'Baadhi ya watu hawa ni wana wapotevu nao wanarudi nyumbani kwa mara ya pili. Malaika wote mbinguni wanafurahia. Mbona ninyi hamfurahii wakati wana wapotevu wanaporudi nyumbani?'

Kwa ufupi, hali na mazingira ya fumbo hili kuu ni mchoro mkuu wa Yesu akisema kwa lile kundi na duara la upande wa nje kuwa, 'Kile ninyi mnakiona tu ni watoza ushuru na wenye dhambi. Hebu mimi niwaambie kile Mungu anachokiona. Mungu anawaona watu kama kondoo waliopotea. Wao hawana mbele wala nyuma, lakini wanaendelea kupatikana huku kote mbinguni kukiwa kumejaa furaha. Mungu anawaona watu waliopotea kama ile sarafu. Mungu anawaokoa na kuwakomboa hao waliopotea njia yao. Anawaona watu ambao waweza kuwa kama nguruwe, lakini wao si nguruwe licha ya kuwa walikuwa wakiishi katika zizi la nguruwe lililopo hapa ulimwenguni. Wao wanatoka katika zizi la nguruwe la ulimwengu huu kwa kuwa ni wana! Mbinguni kote kuna furaha kuu kwa kuwa waliokuwa wamepotea wamepatikana. Mbona ninyi hamfurahii haya?'

Wakati tunapochukua ile hali na yale mazingira ambayo fumbo hili la mwana mpotevu lilifunzwa, twahitajika kutambua kwamba kina kikuu cha fumbo hili ni wakati mwana mpotevu anaporudi. Kuna karamu na sherehe kuu pamoja na kucheza ngoma. Ndama aliyenona anachinjwa. Yule nduguye mkubwa anawasili kutoka shambani. Amekuwa kila mara akifanya kazi ya kuchosha mchana kutwa, kila siku, kwa ajili ya baba yake. Anamwuiza mmoja wa watumishi wao, '*Mambo haya maana yake nini?'* Naye akamwambia, *Naam, ndugu yako amekuja na baba yako amechinja ndama yule aliyenona, kwa sababu amempata tena, yu mzima.'*

Kisha twasoma kwamba huyu nduguye mkubwa alikasirika sana na akakataa kuingia ndani. Hata hivyo, huyu baba ambaye aonekana kuwa ni mkongwe aliyemkimbilia na kumkumbatia mwanawe; ampenda mwanawe mkubwa pia. Yule baba atoka nje na kumsihi mwanawe mkubwa, kwa kumwambia, '*Mwanangu, wewe u pamoja nami siku sote, na vyote*

nilivyo navyo ni vyako. tena, kufanya furaha na shangwe ilipasa, kwa kuwa huyu ndugu yako alikuwa amekufa, naye amefufuka; alikiuwa amepotea, naye ameonekana.'

Fumbo hili kuu linaonyesha mazingira ambayo lilifundishwa. Huyu ndugu mkubwa katika fumbo hili ni lile duara la nje la Mafarisayo na waandishi ambao hawatashiriki na malaika katika furaha ya mbinguni kwa kuwa aliyepotea amepatikana. Yule baba amsihi nduguye mkubwa kuungana nao katika sherehe sawa na vile Yesu alivyokuwa akiwakaribisha viongozi wa dini hili kushiriki naye katika lengo lake kuu la huduma ya kuwatafuta na kuwaokoa wale waliopotea kama inavyoelezwa katika msitari mkuu wa Injili ya (Luka 4:18; 19:10).

Kuna hali kuwa Yesu anatenda hapa vile alivyotenda wakati alipomshauri Petro kumpeleka katika uvuvi (Luka 5:1-11). Ingawa siwezi kuthibitisha jambo hili, naamini kwamba yawezekana kuwa vile alivyokuwa yule mmishionari mkuu ambaye Yesu aliwahi kumwita alikuwa ni mmoja wapo wa wale viongozi wa dini waliokuwepo katika duara la nje - yaani Sauli wa Tarso.

Huku akimweka Yesu kwenye picha akiwa amesimama katikati ya duara ya ndani akiwa amezungukwa na watoza ushuru na watenda dhambi, akiwakaribisha viongozi wa dini kushiriki naye katika wokovu wa roho zilizopotea, ubinafsi, na matumizi ya fumbo hili la kuvutia la Yesu, kwamba pia anakukaribisha kushiriki pamoja naye katika utekelezaji wake wa Sera Ya Nazareti. Kuna njia ambayo tunaweza kusema kwamba Yesu anaeleza madhehebu yote ya wale ambao hukiri kuwa wao ni Kanisa Lake siku ya leo, hasa walio wa Kanisa la Kinjilistii sababu yetu ya kueneza Injili - kushiriki Habari Njema na waliopotea.

Fumbo Mbili Kuhusu Matajiri

Katika sura ya kumi na sita, tunasoma mafumbo mawili ya kuvutia sana ya Yesu Kristo kuhusu matajiri. Mafumbo yote yahitajika kutazamwa katika hali na mazingira ambayo Yesu aliyafundisha lile fumbo la vitu vilivyopotea katika sura ya kumi na tano. Yesu aliyaelekeza mafumbo hayo mawili kwa wanafunzi Wake lakini wakati alipomalizia la kwanza, wale Mafarisayo walikuwa wamedhihakiwa. Hii inamaanisha kwamba walisikia mafundisho na kwamba ilikuwa dhahiri kuwa Bwana alikusudia mafumbo haya mawili kwao pia.

Fumbo la kwanza kuhusu tajiri, lililojulikana kama, 'fumbo la mtumishi mwovu,' linaonekana kuwa kinyume, lakini kwa hakika ni usemi usio kinyume kuhusu kushiriki na Kristo

katika sera ya uongozi Wake wa Nazareti. Hadithi ya pili, ‘tajiri na Lazaro’ ni usemi wa kinyume kuhusu mtu ambaye alikuwa kinyume na tofauti kabisa na yule Yesu aliyekuwa akimshirikisha katika huduma yake.

Fumbo la kwanza linawatatiza baadhi ya watu kwa kuwa wanaamini kwamba katika fumbo hili, Yesu anasifu tabia ya mwenye hila na ujanja. Lakini hawatafsiri vyema. Fumbo lile ni kuhusu mtu ambaye alikuwa mtumishi, au mweka hazina wa shirika lake. Hapa ndipo tunapata moja wapo ya maneno ya muhimu sana katika Agano Jipya. Agano la Kale linafundisha juu ya fungu la kumi na kutoa sadaka, ambazo zinazidi zaka, ilhali pia linawafundisha watu wa Mungu kufanya sadaka ambazo zitawagharimu kitu (2 Samweli 24:24). Lakini unapoingia katika Agano Jipya, neno linalotumika sana ni ‘uwakili.’ Dhana hii ya ‘uwakili’ siyo kwamba umletee Mungu asilimia kumi ya vyote ulivyo navyo au vile unavyovipokea. Uwakili au ubawabu unamaanisha kwamba wewe pamoja ma vyote ulivyo navyo ni vya Mungu. Jambo lililo la muhimu mno ni uwakili. Je! Wewe u wakili mwema wa kile kilicho katika mamlaka yako? Hii ni pamoja na mali zako, talanta, wakati wako, nguvu’ pamoja na karama zako. Au kwa maelezo mengine, cho chote ulicho nacho na alicho nacho.

Kumbuka kwamba fumbo ni hadithi ambayo huambatanishwa pamoja na kweli ile ambayo Yesu alikuwa akifunza. Kweli ambayo Yesu alikuwa akitaka kutufunza ni ya uwakili. Nayo hadithi inayoambatana na kweli hii ni hadithi ya yule tajiri aliyekuwa na bawabu au wakili. Alipaswa habari kuwa wakilki wake amekuwa mlaghai kwa uharibifu au ufisadi na wizi wa mali yake. Yeye anamwambia kwamba atawaleta wahasibu wachuguze vitabu vya hesabu.

Yule wakili anaketi chini na kujisemea mwenyewe. Ajiambia hivi, ‘Hivi sasa mimi ndimi mwenye kuyasimamia mali yake bwana wangu. Lakini punde tu wakati hao wahasibu watakapovichuguza hivi vitabu, mimi nitaachishwa kazi na nitaukosa uwezo wa kusimimia mali ya bwanangu. Nitafanya nini? Anawaza kisha anakata kauli kuwatembelea waliokuwa wadeni wa bwanake.

Mpango wa hila yake ulikuwa kwamba anajiandaa kwa mambo yajayo. Yeye asema hivi, ‘Wakati huu mimi ningali katika eneo moja lile ambalo mimi ni muajiriwa na ninayo mamlaka juu ya mali na fedha ambazo sio zangu. Mimi nitazitumia hizi mali, ambazo si zangu, kwa njia ambayo hata kama nitaachishwa kazi, nitakuwa nimewafanya marafiki ambao kwa hakika wa watanipokea katika nyumba zao na kunikaribisha kwa furaha. Wao watanikaribisha wakati ambapo sitakuwa na mahali pa kwenda.’ Wakati bwanake (yule mwajiri wake - na siyo

Bwana Yesu), anapoyasikia mambo ambayo mtumishi wake alikuwa ametenda, hampi pongezi wala sifa kwa kuwa ni mwenye hila na ujanja tena ni fisadi. Tafsiri mmoja yasema hivi, '*Yeye alipewa pongezi kwa sababu aliyafikiria mambo yajayo au ya hapo usoni.'*

Matumizi Ya Kibinafsi

Ni ukweli upi ambao Yesu anataka kufunza wakati anapotoa hadithi hii? Tafsiri na matumizi ya fumbo hii, kwa hakika yana uzito sana. Yesu anafundisha hivi: 'Wewe ni kama yule mtumishi. Kila kitu ulicho nacho ni cha Mungu. Kazi yako kwa uhakika ni ya uwakili wa kile ambacho umepewa kuwa nacho. Na kama vile wakili huyo alivyofahamu kuwa angeachishwa kazi, pia wewe unahitaji kufahamu kwamba siku moja utafariki dunia nawe utapoteza uwakili wa mali na fedha zote ambazo Mungu ameweka chini ya ulinzi wako. Nawe utakaposikia maneno haya yenye kukuzindua kutoka usingizini, 'hautakuwa tena wakili. Sasa fanya taarifa ya wako.'

Asili ya fumbo hili ni kwamba, yule wakili aliishi kwa hali mbili. Katika hali ya kwanza, alikuwa na uwezo wa uwakili wa mali na fedha za bwanake, lakini pia alifahamu kwamba atakuja kuondoka na kuingia hali nyingine ambapo atapoteza mamlaka ya uwakili wa mali ile. Bado angali katika hali ya kwanza, alitumia uwezo wake juu ya mali kwa njia ambayo alifanya marafiki ambao wangemkaribisha kwao wakati yeye atakapoingia katika hali ya pili.

Jinsi wakili huyo asiye haki hutumia mali ambayo haikuwa yake kufanya marafiki katika hali ile nyingine, sisi twahitajika kutumia yale tuliyo nayo hili kufanya marafiki katika eneo hilo lingine, kumaanisha hali ya uzima wa milele. Wakati 'tutakapoachishwa' kazi au kufariki dunia, tutakuwa na marafiki ambao watatungojea na kutukaribisha katika makao yao ya milele, au kule wanamoishi.

'*Na mwenye hekima huvuta roho za watu* (Mithali 11:30).' Hii ndiyo maana kuu ya mafunzo yaliyomo katika fumbo hili. Tumia kile ambacho umepewa kwa njia ambayo wakati utakapofariki dunia, kutakuwepo na watu katika hali ya umilele ambao watakwambia*, 'wewe ulimpa mmishionari fedha ambazo zilimwesha kufanya safari. Katika safari hiyo, mimi niliweza kukutana na Kristo. Nisingalikuwa hapa kama wewe haungekuwa wakili mwaminifu.'*

Kwa maelezo mengine, fumbo hili linasema kuwa, yale yote uliyo nayo sio yako na kwamba hautaandamana nazo. Lakini unaweza kununua hisa huko mbinguni. Njia moja

ambayo unaweza kununua hisa huko mbinguni ni katika uwakili bora wa mali na fedha zako na kwa njia ambayo, ufalme wa mbinguni utaenezwa na Yesu Kristo kulijenga Kanisa Lake. Watu wanaweza kukaribia Wokovu kwa ufahamu wa neema ya Kristo kwani kwa uaminifu umesimamia yale ambayo Mungu amekukabithi katika mikono yako.

Baada ya Yesu kueleza hadithi hii, anafanya matumizi haya yaliotiliwa maanani sana. 'Yeye aliye mwaminifu kwa kile kilicho kidogo, ni mwaminifu pia kwa kile kingi. Naye yule ambaye hana haki katika yale madogo pia si mwenye haki kwa yale makubwa. Hivyo basi, hamjakuwa waaminifu kwa mali ile mliyo nayo, ni nani atakaye waamini na kuwakabidhi mali ya kweli?'

Matumizi haya yanamaanisha kwamba Mungu hatatubariki kiroho ikiwa sisi sio waaminifu kwa njia ile ambayo tunasimamia mali yetu. Mkazo haupo juu ya kiasi kile tunachomtolea Mungu bali jinsi ambavyo uwakili wetu ulivyo kwa kile tulichokabidhiwa. Uwakili wenye uwazi na uwajibikaji ndio kina na lengo kuu la fundisho hili.

Je! Wewe unashiriki naye Yesu katika utekelezaji wa sera ya uongozi? Je! Wewe unashiriki na Kristo katika utekelezaji wa huduma hii kuu Yake ulimwenguni? Unaweza kutenda hivyo kama mishionari, mwinjilisti, mchungaji, au shahida mwaminifu wa Yesu Kristo. Kulingana na fumbo hili, unaweza pia kutenda hivyo kwa kutumia mapato yako kuwawezesha wale ambao wanashiriki na Kristo katika umishionari, uinjilisti, uchungaji na mashahidi waaminifu Wake.

Kuna njia nyingi za kushiriki na Kristo, lakini swali ambalo ninahitaji kukuuliza ni je! kwa njia ya kweli na uhakika, unaweza kushiriki naye Kristo, katika kutekeleza malengo ya huduma Yake katika ulimwengu wa siku ya leo? Mengi ya mafunzo Yake Yesu yanatuambia kwamba tutaishi katika uzima wa milele kulingana na jinsi tutakavyolijibu swali hilo siku ya leo.

Katika hadithi ya pili kuhusu tajiri, Yeye asema hivi, *'palikuwa na mtu mmoja, tajiri, aliyevaa nguo za rangi za zambarau na kitani safi na kula siku sote kwa anasa. Na maskini mmoja, jina lake Lazaro, huwekwa mlangoni pake, ana vidonda vingi, naye alikuwa akitamani kushibishwa kwa makombo yaliyoanguka katika meza ya yule tajiri; hata mbwa wakaja wakaramba vidonda vyake.'*

Kama unaweza kufikiria hadithi hii kama mchezo wa kuigiza wenye sehemu tatu, kwenye sehemu ya kwanza, una tajiri akiwa amelala ndani ya kasri yake huku amevalia mavazi ya zambarau na kufurahia vyakula bora kila siku. Kila siku alipotoka kwenye nyumba yake, palikuwepo na yule maskini mwombaji amelala pale huku mbwa wakiramba vidonda vyake. Yule tajiri na kila kitu chema katika maisha yake; ilhali maskini alikuwa anaishi maisha duni kabisa. Hili ni sehemu ya kwanza.

Sehemu ya pili ni kifo cha wote wawili. Wote wawili wafariki dunia. Kifo ndicho kinachofanya watu wote sawa. Yule baada ya kufa akiwa kitandani mwake azikwa kwa sherehe na taazima kuu. Yule Lazaro afa akilala nje mwa langa la yule tajiri. Hatufahamishwi kwamba alipata kuzikwa. Hivyo basi, tunaweza kufikiria kwamba wale wafanyi kazi katika idara ya usafi na afya kwa umma walikuja na kuokota maiti yake na kuiweka kwenye mkokoteni. Huenda maiti hiyo ilitupwa huko kwenye takataka nje ya mji wa Yerusalemu, mahali palipofahamika kama 'Gehenna.' Sehemu ya pili ni kwamba, wote wawili wamekufa.

Wakati pazia inapoinuliwa kwa sehemu ya tatu, tunatambua ukweli ambao Yesu anataka kutufundisha wakati anapotueleza hadithi hii. Kwa sasa, watu hawa wawili wako peponi. Yule maskini, Lazaro alikuwa na furaha isiyo na kifani. Yupo kifuani mwa Ibrahimu. Hii inamaanisha kwamba yupo katika ushirika wa karibu na Ibrahimu. Ilhali tajiri yuko jehanamu kwenye moto. Hapo ni mahali pa mateso na ukatili usio na kifani.

Tunasoma kwamba yeye yupo katika mateso. Kuna tofauti kuu hapa, kuna shimo la utenganisho ambalo linawatenganisha hawa wawili. Hakuna jambo ambalo linaweza kutendeka hili kuirekebisha hali jinsi ilivyo. Yule tajiri anapofahamishwa hivyo, anasema hivi, *'Ee, baba Ibrahimu, nihurumie umtume Lazaro achovye ncha ya kidole chake majini, auburudishe ulimi wangu; kwa sababu ninateswa katika moto huu.'* Lakini anajibiwa hivi, *'kati yetu sisi na ninyi kumewekwa shimo kubwa, ili wale watakao kutoka huku kwenda kwenu wasiweze; wala watu wa kwenu wasivuke kuja kwetu.'*

Sasa, baada ya kufahamu hivyo, anahusika sana juu ya ndugu wake watano. Naye anasema, *'Basi, baba Ibrahimu, nakuomba, mtume nyumbani kwa baba yangu, kwa kuwa ninao ndugu watano, ili awashuhudie, wasije wao pia wakafika mahali hapa pa mateso.' Ibrahimu akasema, Wanao Musa na manabii; na wawasikilize wao. Akasema, La baba Ibrahimu, lakini kama akiwaendea mtu atokaye kwa wafu, watatubu.'*

Yesu anadhamini sana Maandiko ya Musa pamoja na manabii wakati Neno laja baadaye kwa yule tajiri, *'Wasipowasikia Musa na manabii, hawatashawishwa hata mtu akifufuka katika wafu.'* Jambo hili linatimika wakati ambapo licha ya kuwa Yesu alifufuliwa katika wafu haaminiwi hata anapoitangaza Injili ambayo inaweza kuwaokoa watu kutokana na tukio hilo la yule tajiri.

Kwa hakika, hii ni hadithi nzuri sana! Haya ndiyo maelezo sahihi kuhusu hali ya uzima wa milele kwenye Biblia. Hapa ndipo tunazoa dhana kuhusu miali ya mto, hukumu ya milele, na kulipishwa kisasi kwa milele na mateso yake. Hii sio funzo la kipekee la Yesu kuhusu kuzimu. Hapo mahali pachafu pa kutupwa takataka nje ya mji wa Yerusalemu ambapo panaitwa, 'Gehanna' paliwakilisha jina ambalo Yesu alilitumia wakati mwingi pamoja na dhana Yake kuhusu peponi. Neno hilo linawakilisha bonde kuu nje ya Yerusalemu ambapo taka za kila namna hutupwa, pamoja na mizoga ya wanyama na maiti za watu wale maskini. Wakati sura zenye giza kuu katika historia ya Kihebrania zilipokuwa zikiandikwa, wazazi wa Kiyahudi walikuwa wakitoa wana wao kama zaka katika bonde hilo. Wakati aliposema kwamba ikiwa sisi tutamwita ndugu kuwa mpumbavu, basi tuko kwenye hatari ya kuzimu', alitumia neno 'Gehanna.' Neno hilo linaonyesha dhana ya takataka. Kulingana na Yesu, kuokolewa kutoka kuzimu kunamaanisha kutoka uharibifu wa maisha.

Hata hivyo, hadithi hii kuhusu tajiri na Lazaro ndio yenye maelezo sahihi kabisa kuhusu mahali pa wale hawajaokolewa. Jambo mbaya zaidi katika maelezo haya ya kuzimu ni kwamba, yule tajiri anakumbuka yale yote yaliyokuwemo ulimwenguni. Yeye ana muda wote kukumbuka maisha yake yote, yamkini miaka hamsini au sitini au labda sabini aliyoishi humu duniani. Alitenda mambo gani katika maisha haya ya ulimwenguni? Aliishi milele katika mateso yatokanayo na swali hilo.

Hadithi hii inafuata nyingine ya wakili mlaghai. Mungu humpa kila mmoja wetu fursa ya maisha haya nasi tu wakili wake - sio fedha tu ambazo kwa hakika zinaweza kuwa sehemu ndogo katika uwakili wake. Maisha, wakati, nguvu, karama, afya ndio maana ya maisha yetu. Swali kuu la umilele ambalo ninakumbana nayo ni, 'Wewe ulilitenda nini nyakati za maisha yako yote?'

Katika fumbo hilo la wakili mlaghai, Yesu anatuuliza hivi, ‘Je! Wewe utashiriki nami katika utekelezaji na utumizi wa sera yangu ya uongozi katika maisha yako na kila kitu ambacho kiko chini ya uwakili wako?’ Hadithi ya pili kuhusu tajiri, ni mfano mkuu wa mtu ambaye alimjibu Yesu kwa sauti kuu, ‘La Hasha!’

Matumizi ya hadithi hii ya pili ya tajiri pia yanatilia mkazo hali ya utu wa kijamii wa Yesu pamoja na huruma ya yule mpendwa tabibu Luka. Tunaposoma hadithi hii, mambo mengi kuhusu hali ya milele yanaelezwa kwa utaratibu na ufasaha mkuu hivi kwamba tunaweza kupuuza hali ya kijamii.

Mtu mmoja kwa jina *Albert Schweitzer* alisema kwamba mafunzo haya ya Yesu ndio yaliyobadilisha maisha yake kabisa. Yeye aliacha vyeo na madaraka yake ya juu pamoja na faraja ndogo ndogo za kibinadamu zilizo mzingira kama mcheza kinanda mashuhuri, mwana falsafa, daktari pamoja na kuwa msomi mkuu wa theolojia huko Uropa, na kuja hadi Afrika kuwa daktari mishionari. Yeye alitenda kazi yake ya udaktari katika kijiji ambapo hapakuwepo na daktari ye yote karibu. *Schweitze*r alisema kwamba aliposoma hadithi hii ya Yesu, haikumchukua muda mrefu kutambua kwamba Lazaro aliyekuwa akilala kwenye lango la yule tajiri ni ulimwengu uliokuwa umejeruhiwa, ambnao umelala langoni mwa maisha yetu.

Schweitzer alipokuwa safarini huku Afrika, alisema kuwa, ‘Afrika ni Lazaro.’ Pia alisema, ‘maisha yako ndio utetezi <u>wako</u>.’ Mimi nadhani ya kwamba msemo huu una uzito mkuu. Kwa maisha yake, aliufanya usemi huo, ‘kile ambacho tunaamini kwa kweli huwa tunakitenda. Cho chote kile kingine kwa hakika ni maneno matupu tu ya dini.’ Nashangaa ikiwa tunamfahamu Lazaro ni nani?

Naamini kwamba changa moto kuu ya mafundisho haya ni kutilia maanani picha yenye usanifu mkuu na sikitiko kuu anayoichora Yesu kuhusu hali ya kupotea milele. Mtazamo huu wa hukumu ya milele unahitajika kutupa hamu hili kuieneza Injili kwa watu wote ambao bado hawajaisikia. Kama alivyokuwa mtume Paulo, twahitajika kuwa na hamu kuu kutokana na kweli tatu ambazo hazibanduki: Mmoja alikufa kwa ajili ya wote, wote wamepotea, na wote ni lazima waisikie Habari Njema (2 Wakorintho 5:13-6:2).

Hata hivyo, matumizi mengine ya hadithi hii, ni matumizi ambayo ni kina kikuu cha Injili ya Luka. Matumizi hayo ndio haya: Je! Wewe na mimi tunaweza kuwa washirika pamoja na

Yesu katika kutimiza na kutekeleza malengo ya huduma Yake humu ulimwenguni kama inavyoelezwa katika sera ya uongozi ya Nazareti? Je! Tutashiriki pamoja naye katika kuwapa vipofu kuona, na uhuru waliofungwa pamoja na kuponya watu wa ulimwengu huu ambao wamevunjika na kujeruhiwa?

Filisofia Tatu Za Maisha

Katika Injili ya Luka, tambua ni mara gapi na ni katika sehemu zipi ambazo Yesu atupa changa moto hili kuwa washirika pamoja naye katika kuitekeleza sera ya uongozi. Inawezekana kwamba kwa sababu Luka ni tabibu, ndio sababu anatupatia hadithi ya kifumbo juu ya msamaria mwema. Yesu anatueleza hadithi ya mtu ambaye alikuwa amevamiwa na kujeruhiwa na wanyang'anyi baada ya kuporwa mali yake na kuachwa kando ya njia afe. Baada ya tukio hilo, aina tatu za watu walipita kando yake na kumwona akiwa mahututi bila matumaini nao wakapita kando mwa njia (10:25-37).

Njia hii ilio katika hadithi hii ilipanda kutoka Yerusalemu hadi Yeriko. Makuhani wakati mwingi walisafiria njia hii hili kwenda mapumzikoni huko Yeriko baada ya huduma nyingi huko Yerusalemu katika Hekalu la Sulemani. Moja baada ya mwingine, wawili kati ya hawa makuhani walipita pale na kushuhudia janga hilo la mtu aliyekuwa hajiwezi na kando mwa njia. Kila mmoja wao huenda alikuwa akisema, 'Kwa hakika kuna shida kuu mahali hapa, lakini nasikitika kwamba sitahusika.' Tunasoma kwamba walipita upande mwingine wa njia na kwenda zao.

Hata hivyo, kulikuwepo na msamaria ambaye alisafiri katika njia hiyo. Alipomwona yule mtu aliyekuwa maututi, alisimama na kutibu majeraha, akampandisha juu ya punda wake na kumchukua hadi kwenye chumba cha wageni. Baada ya kumlipa mwenye nyumba, alimwambia kuwa, *'mtu ze huyu na cho chote utakachogharimiwa zaidi, mimi nitakaporudi nitakulipa.'*

Fumbo hili lilifundishwa kama jibu kwa sawa Yesu aliloulizwa na mwanasheria: 'Jirani yangu ni nani?' Jibu hili lenye uzito sana la Yesu linatupa falsafa au kanuni tatu za maisha au za Jirani. Baada ya kutoa hadithi hii, Yesu alijibu swali la yule mwana sheria ambalo lilikuwa: 'Ni nani kati ya hawa watatu alikuwa jirani wa kweli?'

Kwanza, Yesu alijibu swali la mwana sheria kwa mfano wa wanyang'anyi ambao walikuwa wamemvamia na kumjeruhi yule mtu. Falsafa yao ni hii, 'kilicho changu ni changu, na kilicho chako kitakuwa changu kwa haraka iwezekanavyo.' Kuna watu wengi ulimwenguni ambao wana falsafa kama hii katika maishani yao. Hii ndio sababu tuna serikali na askari, pamoja na wanajeshi.

Yule kuhani na mlawi - watu wa dini katika hadithi hii - ni maelezo ya jibu kwa swali hili na maana ya jirani: *'kilicho changu ni changu na kilicho chako ni chako. Mimi nina baraka zangu nawe una baraka zako. Nina shida zangu nawe una shida zako. Kwa hakika, una shida, lakini falsafa yangu ni hii 'ishi na upate kuishi. Changu ni changu; chako ni chako. Mimi sitahusika nawe!'* Watu wengi wa dini wana falsafa hii ya maisha na jirani.

Kuna jibu la tatu katika hadithi hii kwa swali la Yesu kuhusu falsafa yetu ya kimaisha pamoja na jirani. Bwana wa kipekee wa kuzitumia hadithi za mafumbo aliambatanisha hadithi hii na ukweli ambao alitaka kutufunza. Ukweli huo unadhihirishwa kwa njia ambayo yule msamaria alivyojibu swali la Yesu. Falsafa ya kimaisha ya msamaria na jirani ilikuwa: 'Kilicho chako ni chako na kilicho changu ni chako wakati wo wote ukihitajipo.'

Falsafa ya maisha na jirani haitakufanya kuwa tajiri, ingawa ndio Yake Yesu kuhusu Lazaro aliyekuwa akilala langoni - ulimwengu wa watu ambao ni maskini wa kiroho kwa kuwa wao ni vipofu, na wamefungwa na kuvunjwa moyo.

Unapotembea miongoni mwa watu katika siku ya leo, jifunze kutazama kila mmoja ambaye unakutana naye katika maisha yako kama ni vipofu, wafungwa, pamoja na watu waliovunjika ambao kwa ajili yao, Yesu alikuja ulimwenguni. Jifunze kuwaona watu wa ulimwengu huu kama kondoo, sarafu, wana waliopotea pamoja na yule 'Lazaro Mkuu' aliyelala katika malango ya Kanisa. Kisha, utatambua kwamba Kristo ambaye huishi ndani yako angependa kuwafikia kupitia wewe, na kukufanya kuwa sehemu ya suluhisho na jawabu kwa mahitaji yaliyomo katika maisha haya pamoja na hali ya umilele.

Inasemekama kwamba Kanisa siku ya leo ni kama mchuano wa kombe la duniani. Wakati unaposhiriki au kutazama mchezo huo kwenye runinga, unaona maelfu ya watu ambao kwa hakika wanahitaji mazoezi, na mapumziko mengi, hali wao wakiwatazama watu ishirini na mbili, ambao nao wanahitaji kupumzika baada ya mazoezi zaidi! Unapotilia maanani huduma

ya ulimwengu ya Yesu katika siku ya leo, fanya uamuzi wa kujitolea Kwake anaye hai kuwa hautakuwa tu mtazamaji bali pia utakuwa mshiriki na mchezaji anayetengemewa kufanya wanafunzi kwake Yeye katika kila taifa kuanzia na majirani wako.

Sura Ya Sita
'Mwokozi Mtafutaji'

Hadithi Ya kuvutia Ya Uponyaji (Luka 8:26-39)

Wale ambao wametenda kazi katika hospitali za wazimu kabla ya madawa ya kutuliza akili kuwepo kwa hakika wanaweza kukubali hadithi hii inayogusa sana. Mtu ye yote ambaye amejitolea kwa hospitali hizi zao wagonjwa wa akili kwa hakika anaweza kukitoa cho chote hili kuona yule ampendaye akiwa katika na akili timamu. Wafanyi kazi ambao hutenda kazi pamoja na hawa tunaowatambua kama wagonjwa wa akili, wanaweza kutoa zaidi hili kufahamu jinsi Yesu alivyoponya kwa njia ya mwujiza.

Wakati Yesu pamoja na wanafunzi wake walipokwenda katika nchi ya Wagerasi, walikutana na mtu aliyekuwa na pepo mbaya. Mtu huyu aliyestahili huruma alimwuliza Yesu swali linalogusa sana wakati walipokutana. *'Yesu, nina nini na wewe*? (8:28).' Kuna watu wengi katika ulimwengu huu ambao wana matatizo kiasi kwamba hawafikirii Yesu na wokovu wake unaweza kuwa na maana ye yote kwao. Wao wameteswa mno na ishara zao kiasi kwamba hawawezi kuamini kwamba Yesu huwajali, au anaweza kushiriki katika katika shida na taabu zao. Katika hadithi hii yenye kuvutia, mtu ambaye alikuwa na pepo mbaya aligundua kwamba Yesu na wokovu wana kila kitu kinachohitajika kikinga hali yake mbaya iliyokuwa katika maisha yake.

Kuna ujumbe mwingine katika hadithi hii yenye kuvutia. Baada ya kuponywa, wakati Yesu alipokaribia kutoka huko, mtu huyo alitaka kuingia kwenye chombo na kusafiri na Yesu. Tunaweza kufikiria kwa urahisi sababu yake kutaka kusafiri na kutoka mahali hapa ambapo kila mtu alifahamu ishara za kutisha katika kipindi cha miaka mingi ya mateso. Tunaweza kutambua ni sababu gani ambayo angependa kuwa na Yesu.

Lakini, anaambiwa hivi, '*Rudi nyumbani kwako, ukahubiri yalivyo makuu Mungu aliyokutendea!* (8:39).' Tafsiri nyingine inasema kuwa, alikuwa aonyeshe mambo makuu

ambayo Mungu alikuwa amemtendea. Mtu huyu ambaye ni muijiza, ni mmishionari wa Yesu kwa wale ambao ni wa nyumba yake na wanaomfahamu vyema.

Hii inafafanua maana ya mmishionari. Ikiwa Mungu amekutendea mambo makuu, kwa hakika u mmishionari. Kama mshumaa juu ya kinara chake, au mji uliojengwa juu ya mlima na ambao hauwezi kusitiriwa, sisi twahitajika kuonyesha na kuhubiri mambo makuu ambayo Mungu ametenda kwetu. Wajibu huu wa umishionari unahitajika kuanza pale ambapo ni pagumu zaidi, pale ambapo twafahamika vyema zaidi, na pale ambapo itamaanisha zaidi - nyumbani kwetu.

Muijiza huu kwa hakika, ni kutoa pepo mbaya. Yesu anahusika moja kwa moja na kumzungumzia yule pepo mbaya katika mtu huyo. Je Yesu angelimtibu mtu kama huyu kwa njia nyingine tofauti kama angekuwepo duniani siku ya leo? Je, Yeye alimtaja huyu mtu kama mwenye 'ugonjwa wa akili wenye utu uliogawanyika na kufedheheshwa', na kumweka katika hospitali wanapofungiwa, na kupewa madawa ya kutuliza akili? Je! Wewe unafikiria nini?

Mafarisayo Na Watoza Ushuru (Luka 18:9-14)

Hapa tunao watu wawili, maombi mawili, hali mbili na matangazo mawili. Jambo lililo muhimu kuhusu hawa watu wawili ni kwamba, mwishoni mwa hadithi, mmoja wao alitangazwa na Yesu kuwa 'amefanywa haki' naye yule mwingine hakutangazwa hivyo - au mmoja wao aliokolewa ilhali yule mwingine hakuokolewa. Njia nyingine ya kusema hayo ni kwamba, mmoja wao alikuwa katika hali ya neema naye yule mwingine hakuwa katika hali hiyo

Neno 'kufanywa haki' linamaanisha, 'kana kwamba sikuwahi kutenda dhambi.' La ziada katika jambo hili, linamaanisha kwamba, Mungu ametutangaza kuwa wenye haki. Kitabu cha Warumi kitatuambia, katika njia ya ufasaha na kwa urefu, jinsi Mungu hutenda jambo hillo. Katika fumbo hili, Yesu anatupasha Habari Njema ambayo ni ya kweli. Kulingana na Yesu, njia ya kuhesabiwa haki ni kuomba jinsi mtoza ushuru alivyoomba: *'Ee Mungu, uniwie radhi mimi mwenye dhambi.'*

Tunasoma kwamba yule Farisayo aliomba 'Na yeye mwenyewe.' Maombi yake yalianza na yeye mwenyewe, yalikuwa kuhusu yeye mwenyewe, na yalimalizika na yeye mwenyewe. Hayakusonga mbali na yeye mwenyewe. 'Kuomba' humaanisha, kuuliza.'

Kufafanua hilo, yule Farisayo hakuomba hata kidogo kwa sababu hakumwuliza Mungu cho chote.

Fumbo hili lilielekezwa kwa wale ambao walijitumainia wenyewe kwamba wao ni wenye haki na kuwadharau wale wengine. Ni jinsi gani ambayo mwenye dhambi afanyika kuwa mwenye haki? Je! Ni matokeo ya jitihada yetu wenyewe? Je! Mimi ni mwenye haki au huhesabiwa haki kwa sababu natengemea jitihada yangu mwenyewe hili kuwa haki? Fumbo hili linasema kuwa, 'La Hasha!' Mungu atanihesabu kuwa 'kana kwamba sikuwa nimetenda dhambi,' wakati ninapokiri kuwa mwenye dhambi, na kwamba siwezi kujiokoa mwenyewe, kisha namwuliza anirehemu.

Katika fumbo hili, Yesu anatangaza Habari Njema ambayo ni ya kweli! Kila mwanamume, mwanamke, mvulana, au msichana ulimwenguni anaweza kuhesabiwa haki ikiwa ataitwaa hali ya unyenyekevu, kuvunjika moyo, kukiri, pamoja na toba wakati anapoomba na kusema, *'Ee Mungu niwie radhi mimi, mwenye dhambi!' H*ali ambayo alichukua Farisayo ilikuwa kinyume kabisa na hali ya maombi ambayo ni ya unyenyekevu, kuvunjika moyo, na kukiri pamoja na toba ambayo huweka na kutudumisha sisi katika hali ya neema.

Msomi mmoja mcha Mungu aliamini kwamba Zakayo, mkuu wa watoza ushuru, ambaye tunakutana naye katika sura inayofuatia, kuwa alikuwa mtoza ushuru ambaye anatajwa katika fumbo hili. Msingi wake uko katika ukweli kwamba Yesu alimwita kwa jina lake, kumaanisha kwamba walifahamiana mmoja kwa mwingine. Hii pia inaweza kumaanisha kwamba Yesu alikuwa akienda huko Yeriko 'kufuatilia' ombi la huyu Zakayo - hili kumweleza zaidi maana ya toba na jinsi ambayo ingetekelezwa katika maisha yake. Ilimbidi kupeana mali yake, iliyomjia kwa njia ya udhalimu. Ingawa haya ni mawazo tu, yanatuongezea shauku katika hadithi moja yenye kuvutia katika Agano Jipya.

Yesu Pamoja Na Mkuu Wa Watoza Ushuru (Luka 19:1-10)

Tunaposoma sura za kumi na nane na kumi na tisa ya kitabu cha Luka, tunagundua hadithi nyingine mbili kuhusu matajiri. Pia tunaweza kuelezea mahojiano ya Yesu na yule mtoza ushuru Mkuu kama mchezo wa kuigiza wenye sehemu tatu. Sehemu ya kwanza ni pale Yesu anamsalimia Zakayo. Sehemu ya pili inatokea katika nyumba ya Zakayo, pale ambapo Yesu ameshida siku kutwa katika mazungumzo na ushirika pamoja na mtu huyo aliyechukiwa sana na kila mtu huku Yeriko.

Pazia inapofunguliwa katika sehemu ya tatu, huku Yesu na Zakayo wanatoka ndani ya nyumba baada ya kuwa pamoja mchana kutwa. Maneno ya kwanza yanazungumzwa na Zakayo. Yeye anamwita Yesu 'Bwana' na kutangaza kwamba atatoa nusu ya mali yake kwa maskini na kutumia ile nyingine kulipa mara nne wale aliokuwa amewanyang'anya huko Yeriko. (kama hangekuwa amenyang'anya ye yote, basi hangedhania kwamba ingegharimu nusu ya mali yake kutatua shida hiyo.)

Sehemu ya pili ndio muhimu sana katika 'mchezo huu.' Sisi hatufahamu cho chote ambacho kilitukia katika sehemu ya pili, au katika nyumbani kwa Zakayo. Je! Wao walizungumza mambo gani siku kutwa? Ni lazima kwamba walizungumzia kuhusu toba, msamaha na jinsi ya kumfuata Yesu. Mazungumzo hayo ni lazima kwamba yalihusu fedha, kwa sababu ya yale maneno yaliyozungumzwa kwanza na Zakayo. Ni wakati Yesu anaposikia hayo maneno kutoka kwa mwenye dhambi huyo mkuu wa Yeriko anapomtangaza kuwa mwana wa Ibrahimu, kwamba ameingia katika nyumba Yake siku hiyo.

Sehemu iliyo bora kwangu katika hadithi hii ni wakati Yesu anaamua kutumia siku hiyo huko Yeriko pamoja na mwenye dhambi huku watu wale wengine wakinung'unika kuhusu jambo hilo. Ningependa kumtafuta msanii achore Yesu, ambaye kulingana na historia ya Myahudi mmoja kwa jina Josephus, alikuwa mtu mashuhuri akitembea nyumbani huku mkono wake ukiwa mabegani mwa Zakayo, ilhali watu wote wenye 'haki' wakinung'unika kwa sababu Yesu alikuwa siku kucha huko Yeriko pamoja na mkuu wa watoza ushuru.

Maneno yenye kuvutia ambayo yanamalizia hadithi hii yanaweza kuandikwa chini ya shaba hivi: '*Kwa Mwana wa Adamu ambaye alikuja kutafuta na kuokoa kile kilicho potea!'* Maneno haya ni mojawapo ya mistari ambayo ina ufafanuzi katika Injili ya tatu ambayo inatupatia usemi katika maisha yaliyo muhimu kuwahi kuwepo ulimwenguni (19:10).

Pia tunaona mpango wa Yesu katika mahojiano haya. Alikuwa akipitia tu Yeriko, na mpango wake ni dhahiri kwamba ni kuwafikia watu ambao wangeweza kuufikia mji wa Yeriko kwa ajili Yake baada ya kupita mji huo na vitongoji vyake.

Hebu jaribu kufikiria jinsi na hali ya mji huo baada ya Zakayo kuanza kuwatembelea watu ambao alikuwa amewatoza ushuru zaidi, yamkini akiongozea bakshishi ndogo juu yake

jinsi walivyotenda watoza ushuru kwa wakati mwingi. Hebu shuhudia mshangao wao, furaha na butwaa huku wakidhania kwamba alikuwa anataka kuingia katika pochi au mifuko yao hata zaidi, hasa walipogundua kwamba alikuwa akitaka kuwalipa mara nne ya kile alichokuwa amechukuwa kutoka kwao; kwa kuwa alikuwa amekutana na Yesu! Naweza kufikiria kwamba hili lilikuwa tukio moja kuu tangu wakati kuta zilipoanguka chini nyakati za Yoshua.

Mazungumzo Mengine Na Tajiri (Luka 18:18-27)

Kuna hadithi nyingine kuhusu tajiri katika sura iliyotangulia ambayo inastahili kufuatia hii ya Yesu na Zakayo. Unapolinganisha au unapotofautisha watu hawa wawili matajiri, jambo la kwanza hebu tazama usawa waliokuwa nao:

Wote wawili walikuwa matajiri. Wote wawili walikuwa Wayahudi. Wote wawili walikuwa na hamu kuu kumwona Yesu. Zakayo alipanda juu ya mti, ilhali mwenzake alimjia Yesu akikimbia na kupiga magoti mbele Yake. Wote wawili walimjia Yesu mbele ya makutano. Ni wazi kwamba wote wawili walikuwa na hamu kujua jinsi ya kuokolewa, au jinsi ya kuwa na uzima wa milele. Ni dhahiri kwamba Yesu aliwapenda wote wawili. Na pia, ni dhahiri kwamba Yesu alikuwa amewaambia wote kutubu dhambi zao na kudhihirisha toba yao kwa kutoa mali yao.

Unapotofautisha hawa wawili, hebu tazama tofauti zao jinsi zinavyoshangaza: Yule kijana mdogo alikuwa mwenye dini na tabia njema, ilhali Zakayo alikuwa hana dini na mdhalimu. Yule kijana angeheshimika katika jamii, ilhali twaambiwa wazi kabisa kwamba sivyo kwa Zakayo.

Tofauti kuu na yenye umuhimu kati ya hawa wawili ni kwamba, Zakayo alitubu dhambi zake na kutoa mali yake, ilhali yule kijana hakutubu. Ingawa yule kijana alikuwa mwenye sifa njema, hakuokolewa, ilhali Zakayo aliokolewa! Yamkini inawezekana kwamba yule kijana alipata kutubu baadaye licha yetu kudhani kwamba alikufa akiwa mwenye tabia njema, lakini mpotevu. Hii inamaanisha kwamba ingawa Zakayo alikuwa mouvu na dhalimu kabla ya kukutana na Yesu, sasa yuko mbinguni siku ya leo, ilhali yule kijana tajiri, yuko Jehanamu!

Ni vyema ikiwa hatutakosa kuelewa hadithi hii. Yesu hasemi kwamba tunaokolewa kwa kile matendo yetu, au kile tusichotenda. Yeye anatufunza kwamba, wakati tunapookolewa

kikamilifu, tunatubu dhambi zetu na kuziacha. Tunaona jambo hili kuwa dhahiri sana, yenye ulinganifu na tofauti wa watu hao wawili na jinsi walivyompokea Yesu.

Hadithi ya Yesu na Zakayo kwa hakika inaanza na mafumbo ya yule Farisayo na Mtoza Ushuru. Tunaposoma fumbo ambalo linafuatia, tunapata kifungu kingine cheny ufafanuzi ambacho kinaelezea Yesu kama mwokozi anayetafuta na ambaye kwa hakika ndivyo alivyo. Tunaona picha ya Yesu pamoja na ile hati ya sera ya uongozi kwa mara ya mwisho wakati Luka anapotupatia mtazamo wake wa mwaliko mkuu mwisho wa Injili hii (Luka 24:46-49).

Maneno Ya Mwisho
'Mawazo Ya Ukristo'

Yesu alitoa mafunzo mengi kama 'fumbo la mpanzi,' ambalo linatuambia jinsi ya kusongea na kupokea mafunzo Yake. Luka ananakili mafumbo matatu ambayo Yesu alitumia kwa sababu hiyo (Luka 5:36-39; 7:21-35). Ya kwanza mawili ni kuhusu kipande cha vazi mpya ambacho kimetiwa kama kiraka kwenye vazi kuu kuu, na divai mpya kuwekwa katika vibuyu vya ngozi kuu kuu.

Watu waliokuwa wakimsikiliza Yesu walifahamu yale mafumbo kwa kuwa yalikuwa ni mambo ya kawaida kila siku, na mifano yenye uzito sana. Kila mwanamke aliyeshonea kiraka juu ya vazi alifahamu kwamba mtu hashonei kiraka kipya juu ya vazi kuukuu. Kiraka kile kipya chenye nguvu kingelifanya lile vazi kuukuu kuzudi kupasuka.

Inawezekama kwamba miongoni mwa wasikilizaji wengi walikuwa wamefanya makosa ya kuweka divai mpya, katika viriba kuukuu. Huku divai hii mpya ikichachuka, vile viriba hupasuka. Kisha baadaye ile divai itamwagika na vile viriba kuharibika.

Matumizi ni kwamba, mafunzo ya Yesu (kama kile kiraka kipya na divai mpya) iyataweka ushawishi juu yetu wakati tunapoyatia ndani ya mawazo yetu. Wale ambao ni viumbe vipya kutokana na kuzaliwa mara ya pili ni dhahiri kwamba wao ni 'ngozi viriba mpya vya divai' ambavyo vinatiwa 'ile divai mpya' ya mafunzo yake ni lazima yamwagwe (2 Wakorintho 5:17). Ni viumbe hawa wapya ambao waweza kuelewa, kupokea na kutimiza mafunzo yake, jambo ambalo laonekana kuwa matumizi ya mafumbo haya.

Ikiwa hatuwezi kujitolea kwa ushawishi ambao unatokana na mafunzo haya kwa mapenzi na mawazo yetu, kwa hakika tutalipuka mawazoni mwetu! Hii ndio sababu Yesu anatuambia tusiwe watu wenye 'nia mbili za kiroho' kwa kujaribu kutumikia mabwana wawili (Mathayo 6:24). Ikiwa hatutasongea na kupokea mafunzo ya Yesu kwa kujitolea na kutii mafunzo yake, kile mtume Yohana anachotaja kama 'uvugu-vugu' wa maungamo yetu ya imani katika Kristo, yatatufanya kuwa wagonjwa, na kumfanya Kristo aliyefufuka kuwa mgonjwa wakati anapowazia juu yetu (Ufunuo 3:15, 16).

Yesu alitumia mafumbo hayo matatu hili kuzungumzia kuhusu jinsi viongozi wa kidini walivyokataa mafunzo na mahubiri ya Yohana Mbatizaji (7:31-35). Watoto walicheza michezo sokoni kama 'harusi' na 'mazishi' kwa kuwa wao walishuhudia hayo. Wao wangewauliza wafanyi biashara wenye shughuli nyingi kusimama na kucheza michezo hiyo pamoja nao.

Kwa mafumbo haya, Yesu alikuwa akisema kwamba Waandishi na Mafarisayo walikuwa kama watoto wadogo wakimwuliza Yeye kucheza na 'mazishi' kwa kuwa aliwaonyesha mfano wa baraka, au mtu mwenye furaha. Wao walikuwa wakimwuliza Yohana Mbatizaji kucheza 'harusi' kwa kuwa alikuwa mtu mwenye juhudi nyingi na haki katika maisha yake ya kiroho huko nyikani, akihubiri kuhusu toba.

Jambo ambalo Yesu alikuwa akionyesha lilikuwa kwamba Yeye na Yohana hawakuwa wamekuja kucheza mchezo huo wa watoto. Haukuambatana na mafunzo yao kwani walikuwa wamekuja kupindua kabisa mafunzo yale ya dini yaliyokuwa yamekolea.

Kwa sasa, umefahamishwa kwa mafunzo yaliyo na uwezo mkuu ya Yesu Kristo. Je! Utaitikia yale uliyojifunza katika ukaguzi huu Injili ya Luka kwa njia gani? Utatenda nini kuhusu kile unachofahamu kuhusu malengo makuu ya huduma ya Kristo aliyefufuka? Lengo na kusudi la mafunzo Yake ni kubadilisha mawazo, maisha na thamani zako. Yesu alituonya kwamba ikiwa hatutafanya lo lote kutokana na mafundisho yake, 'maono yetu ya kiroho' yatalipua mawazo yetu.

Injili ya Yohana inatupatia nakala mwafaka kuhusu kufa na kufufuka kwa Yesu. Kwa kuwa nina vitabu sita ambavyo vinayatoa maelezo na fafanuzi katika vipindi mia moja na thelathini kwenye radio, juu ya Injili ya Yohana, sitazungumzia sana kuhusu sehemu hii

muhimu ya maisha na huduma Yake, iliopo katika vitabu hivyo. Jambo la muhimu kuhusu kifo chake ambacho sisi tunakipokea katika kitabu cha Luka ni pale Yesu anawaambia mitume kwamba Pasaka itatimizwa wakati atakapofariki juu ya msalaba (22:16). Isipokuwa Yohana pekee, waandishi wa Injili wanatuambia kwamba 'walimsulubisha' wakati wanapotaja kifo cha Yesu Kristo juu ya msalaba.

Ikiwa haujamfahamu Kristo kuwa kama mwokozi wako binafsi, kama mhudumu wa Injili Yake, nakusihi kutambua kwamba Yesu alikuja hili kuondoa upofu wako, na kukufanya huru kutokana na ulevi na tabia za dhambi. Yeye anataka kuponya moyo na maisha yako yaliyovunjika, kama Mwokozi wako binafsi. Pia, anataka kukuletea kusudi kuu katika maisha yako huku akikufanya mshiriki pamoja naye katika huduma Yake kuu ya kuwatafuta na kuwaokoa wale waliopotea. Mtumainie wakati huu awe Mwokozi wako. Mfanye kuwa Bwanako, kisha tumia maisha yako yote katika uhusiano naye Kristo aliyefufuka ukitekeleza ile sera kuu ya uongozi katika ulimwengu.

INJILI YA YOHANA

Sura Ya Saba

'Lugha Ya Ishara Ya Yohana'

Katika vitabu vile vingine sita, ninatoa maelezo kwa wasikilizaji wetu ambao wamesikiliza vipindi mia moja na thelathini katika redio ambavyo hufundisha kuhusu Injili ya Yohana, msitari mmoja baada ya mwingine. Katika kitabu hiki ningetaka kutoa baadhi ya maandishi kwa wale ambao wamesikiliza vipindi ambavyo hupeana ukaguzi mfupi wa Injili ya nne kama sehemu ya uchuguzi wa Agano Jipya.

Sasa, tunakaribia kitabu nikipendacho zaidi katika hizi Injili nne. Injili ya Yohana ndio huvutia mamilioni ya watu kwani Mungu ameitumia kuwaletea imani ndani ya Kristo. Mimi huvutiwa sana na mfumo wa uandishi ambao Yohana ametumia kuandika Injili yake. Hii pia imetokea kuwa Injili niipendayo sana kwani kusudi la Yohana katika uandishi wa Injili hii ni lile toleo na mfumo anaotupatia katika sura ishirini na mmoja, ambazo zinaelezea kuhusu Yesu Kristo. Hii ndio Injili inayovutia zaidi kwa sababu sio tu kwamba Yohana anaonyesha jinsi ya kuokolewa bali kupitia kuisoma, unapata kumjua Mwokozi ambaye hukoa.

Mtume Yohana ambaye aliandika kitabu cha Ufunuo, ndiye pia mwandishi wa Injili hii. Ikiwa unafahamu kitabu cha mwisho katika Biblia, basi una ufahamu wa mfumo wa uandishi wa Yohana. Wakati Yohana alipoandika kitabu cha Ufunuo, alitumia neno ambalo hutusaidia kufahamu mfumo wa uandishi wake. Anapoanza kitabu hicho cha mwisho katika Agano Jipya, anaandika hivi: *'Ufunuo wa Yesu Kristo, aliopewa na Mungu awaonyeshe watumwa wake mambo ambayo kwamba hayana budi kuwako upesi; naye akatuma kwa Mkono wa Malaika akamwonyesha mtumwa wake Yohana.'*

Yohana anatumia neno lenye kuvutia sana, 'akamwonyesha' wakati anapoandika Ufunuo ambapo Injili hii inatujulisha kwamba aliandika 'lugha ya ishara' ya Kibiblia.

Mtume Paulo aliandika kwamba Injili ilikuwa ni upuzi kwa Wayunani kwa kuwa wao walikuwa watu wenye shauku kuu ya maarifa, na kwamba 'walikuwa wakitafuta ishara.' Paulo alimaanisha kwamba Wayahudi walimwomba Mungu wakati mwingi kuwapa ishara hili kuthibitisha kwamba Yeye alikuwa pamoja nao na kwamba alikuwa akiwaongoza (Mathayo 12:38-42). Pia alikuwa akimaanisha kwamba wakati mwingine, Wayahudi walifikiri na kuwasiliana kwa njia ya 'lugha ya ishara.'

Kitabu cha Ufunuo kimevuviwa, na kina mafundisho yenye uzito mkuu. Kimeandikwa kwa lugha ya ishara ya Keibrania. Ingawa lugha hii ya ishara sio wazi, Yohana anatumia mfumo huo huo katika Injili hii.

Funguo Kwa Injili Ya Yohana

Wakati Yohana anaandika vitabu hivi viwili katika Agano Jipya (Injili ya Yohana na kitabu cha Ufunuo), ni wazi kwamba anaandika jumbe kwa watu wa Mungu kupitia ishara zilizovuviwa. Na wanaposoma jumbe hizo, watu wa Mungu huhitaji 'funguo ambazo hufungua mihuri.' Baadhi ya 'funguo' ambazo zinaweza kukusaidia 'kufungua zile ishara' za lugha kuu ambazo Yohana anatumia katika Injili hii.

Ufunguo Wa Kwanza

Ufunguo wa kwanza wa kuifahamu Injili hii ni kutambua kwamba asilimia tisini (90%) ya yale yaliyo ndani yake hayapatikani katika Injili zile zingine tatu za kwanza. Tunaposoma Injili hii, tunahitaji kutambua kwamba Yohana ana mtazamo wa kushiriki nasi kuhusu maisha ya Kristo ambayo hayapatikani katika Mathayo, Marko, na Luka. Hivyo basi, tunahitaji kutarajia

kusoma hadithi ya historia ya maisha ya Yesu ambayo ni tofauti na hadithi tulizosoma katika Injili tatu za kwanza.

Ufunguo Wa Pili

Ufunguo wa pili ambao utatusaidia kufungua ishara za ujumbe huu wa Injili ya kipeke ni kutambua kwamba Injili ya Yohana ndio kitabu cha pekee katika Biblia ambacho kimeandikiwa watu wasioamini hili kuwaleta kwa imani na uzima wa milele.

Mtume Paulo anaandika kwamba kusudi la Biblia nzima ni '. . .*hili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema* (2 Timotheo 3:16-17).' Hivyo basi, ni wazi kwamba Biblia haijaelekezwa kwa watu wasioamini, bali kwa wale wanaoamini.

Katika Biblia, kwa hakika Mungu ana ujumbe mmoja tu kwa mtu asiyeamini: Ujumbe huo ni kutubu na kuamini Injili. Hata hivyo, wakati asiyeamini anapotubu na kuamini, Mungu ana vitabu sitini na sita vilivyo vuviwa na vilivyojaa ukweli kwa ajili yake kwa sababu anataka waaminifu kujihami kwa kila kazi njema. Yeye hukusudia kufanya kazi kupitia maisha yao. Mungu hutaka kila mmoja wa waaminifu kukua kiroho na kukamilishwa kuwa watu ambao amewaumba hili kufanyika wapya (Waefeso 2:10; 4:12).

Injili ya Yohana ni kwamba ujumbe mmoja wa Mungu kwa asiyeamini, wahitajika kutoka kwa wote ambao anataka kuwaambia kupitia vile vitabu sitini na tano katika Biblia. Ingawa kuna kweli yenye uzito mkuu katika Injili ya nne ambayo humkamilisha mwaminifu, hiki ndicho kitabu cha pekee katika Biblia ambacho ni wazi kwamba kimeelekezwa kwa wale wasioamini kwa shabaha ya kuwaleta katika imani ya Yesu Kristo.

Yohana anatupatia sababu ya kuandika Injili hii yenye uzito mkuu kuwa: *'Basi kuna ishara nyingine nyingi alizozifanya Yesu mbele ya wanafunzi wake, zisizoandikwa katika kitabu hiki. Lakini hizi zimeandikwa; hili mpate kuamini ya kwamba Yesu ndiye Kristo, Mwana wa Mungu; na kwa kuamini mwe na uzima kwa jina lake* (Yohana 20:30-31).'

Tafsiri moja ya hivi karibuni ina maelezo yaliyo chini ya ukurasa ambayo yanasema hivi: 'Ishara ni muijiza wa kuthibitisha ambao huelekeza kwa uwezo wa Mungu katika neema ya ukombozi.' Hivyo basi, ishara ni muijiza ambao unathibitisha kwamba Yesu alikuwa Masihi, Kristo, Mwana wa Mungu na Mwokozi wa ulimwengu.

Katika msitari wa mwisho wa Injili hii, Yohana aliandika kwamba ikiwa ishara hizi zote za Yesu zingenakiliwa, Ulimwengu haungekuwa na nafasi ya vitabu ambavyo vingeandikwa hiyo miujiza. Hebu jaribu kuvumbua jinsi ambavyo vitabu vingeandikwa kuhusu maisha, miujiza na ushawishi wa Yesu Kristo, nawe kwa hakika, utatambua ukweli uliopo katika utambulizi huu wa Yohana kuhusu Yesu.

Yohana anataka tuchuguze nakala hii ya ishara ambazo zinathibitisha matamshi kuhusu Yesu. Kwa hakika, yeye anaandika hivi: '*Kutokana na ishara ya miujiza mingi ambayo Yesu aliyotenda, tilia maanani - na kwa wazo iliyo wazi kabisa - yale niliyonakili katika kitabu hiki. Hii inaweza kukushawishi kwamba Yesu Kristo wa Nazareti ndiye alikuwa Masihi, Mwana wa Mungu. Ningependa uamini hili kwa sababu, wakati utakapoamini ukweli huo kuhusu Yesu Kristo, utazaliwa kwa mara ya pili nawe utapokea uzima wa milele* (20:30,31; 1:12,13).'

Wakati watu wanapomwambia mchungaji kwamba wangependa kuanza kusoma Biblia, na kuuliza ni wapi ambapo wanahitajika kuanzia, mchungaji anaweza kuwauliza hivi, 'Je! Wewe ni mwaminifu?' Ni kwa sababu Yohana alimwandikia mtu asiyeamini wakati wao wanapojibu, 'La, lakini mimi navutiwa.' Mchungaji wakati mwingi atasema, 'Anza kusoma Biblia katika Injili ya Yohana.' Wachungaji wakati mwingi hupeana ushauri huo kwa sababu Yohana alisema sababu ya kuandika kwake Injili ilikuwa kwamba yule asiyeamini apate kufanyika mwaminifu na kuwa na ujuzi wa milele.

Ufunguo Wa Tatu

Ufunguo mwingine wa kufahamu Injili ya Yohana ni kutambua kwamba Injili hii inatupatia hoja ya kithiolojia kuhusu Yesu. Injili za Mathayo na Luka zinatueleza mpangilio mwafaka wa huduma ya Yesu wanapoinakili hadithi ya historia ya Yesu iliyovuviwa. Hata hivyo, hoja ya Yohana yenye ufasaha na taratibu zenye ushawishi mkuu ni kwa muhtasari na utaratibu unaolingana katika sura ishirini na moja.

Kusudi la Injili hizi nne ni kutuambia kwamba Yesu alikuja. Hali kwamba Mathayo alimdhihirisha Yesu kama Mfalme wa mbinguni, naye Marko akamdhihirisha kama Mtumishi, Mwana wa Adamu, huku Luka akitilia mkazo juu ya utu wake wa kibinadamu, ilhali lengo kuu la Yohana lilikuwa kwamba Yeye alikuwa Mungu.

Taratibu ya hoja ya Yohana ni kwamba Yesu ndiye Kristo, Masihi aliyeahidiwa, Mwana wa Mungu. Ufuatilie ukweli huo kote katika Injili ya Yohana, kuanzia sura ya kwanza, hadi ya mwisho wa Injili hiyo, nawe utaona kwamba katika kila sura baada ya nyingine, Yohana anaendelea kutilia mkazo hoja hii: Yesu wa Nazareti aliyekuwepo katika historia, ndiye Kristo, Mwana wa Mungu na Mwokozi wa Ulimwengu.

Yesu Kristo hakuwa na majina mawili kama mtu anayeitwa '*John Brown.'* Yesu, ndio jina lake; Kristo lilikuwa cheo chake. Sisi tunapomtaja kama 'Yesu Kristo' huwa tunasema kwamba Yesu, aliyetoka Nazareti na aliyepo katika historia, ndiye Kristo. Neno la Kiyunani 'Kristo' ndio njia ya Wayunani ilhali Waebrania husema 'Masihi.' Wakati Yohana anapotuambia kwamba Yesu ndiye Kristo, huwa anatuambia kwamba Yesu tunayetana naye katika Agano Jipya, ndiye Masihi ambaye alitabiriwa katika Agano la Kale.

Katika kitabu cha Matendo ya Mitume, tunajulishwa katika safari za umishionari wa mtume Paulo, ambaye alikuwa Rabi, kuwa alikwenda katika Sinagogi kutoka mji moja hadi mwingine na kuhojiana kwa Maandiko na Rabi wa Kiyahudi ambao alikutana nao, kwamba Yesu ndiye Kristo (Matendo 17:2,3). Katika nyaraka za mtume Paulo, anatuambia kwamba fundisho kuu la ushirika katika Kanisa la Agano Jipya lilikuwa '*Yesu ndiye Bwana* (1 Wakorintho 2:22; 5:1).' Hoja ambayo Yohana anaeleza katika mistari hii miwili na mifupi katika waraka wake wa kwanza ndio ile ile ambayo alieleza kwa taratibu katika Injili hii.

Ufunguo Wa Nne

Kulingana na funguo tatu za kwanza katika Injili hii, hii ndiyo njia ambayo nashawishiwa kwamba twahitajika kusoma Injili ya Yohana. Twahitajika kusoma sura zote ishirini na moja tukitatufa majibu kwa maswali haya matatu: Yesu ni Nani? Imani ni nini? Maisha ni nini?

Yohana aliandika Injili hii yake hili kutupatia nakala ya ishara, au miujiza ya kuthibitisha aliyoitenda Yesu, ambayo yeye aliichagua kwa sababu anataka kutushawishi kwamba jibu kwa swali lile ni kwamba, Yesu ndiye Kristo, Masihi, Mwana wa Mungu. Katika sura moja baada ya nyingine, Yohana atatuonyesha na kutuambia katika njia nyingi za kuvutia kwamba Yesu ndiye Kristo, Masihi na Mwana wa Pekee wa Mungu. Yohana ataeleza kweli hii ya msingi katika njia nyingi kwa kila sura ishirini na moja zake.

Katika kila sura, twahitajika kutafuta jawabu kwa swali hii: Imani ni nini? Yohana aliandika hivi: *'Nitawaambieni ninyi haya mambo kumhusu Yesu. Ikiwa mtayaamini, ninyi mtazaliwa mara ya pili na kuupokea uzima wa milele* (20:30,31; 1:12, 13).' Katika kila sura, Yohana hatatupatia tu changa moto hili kuamini mfumo sanifu wa hoja yake kuhusu Yesu. Pia, atatuonyesha kile anachomaanisha kwa imani, wakati atakapotuhimiza kuamini ile hoja yake kuhusu Yesu ni nani.

Imani kwa hakika ni nini? Imani ni dhana iliyo ngumu sana kufafanuliwa na kuweka katika mtazamo. Hivyo basi, katika sura baada ya sura nyingine, na kwa njia nyingi zinazovutia, Yohana atatuonyesha maana ya kuamini Yesu ndiye Kristo.

Katika kila sura, Yohana pia atatuonyesha na kutuambia kile anachomaanisha kwa uzima wa milele. Uzima wa milele sio kwamba ni uzima usio na mwisho tu. Atalitumia neno hilo pia, lakini uzima wa milele sio tu wingi wa uhai, bali kwamba ni thamani ya maisha. Yohana anaandika kwamba Yesu alisema hivi, '*Mimi nimekuja wawe na uzima kisha wawe nao uzima tele* (Yohana 10:10).' Je! Hii thamani ya maisha haya ya uzima tele ambayo Mungu ameyafanya, na kwa sababu hiyo, anatarajia wanadamu kuwa nao ni gani?

Thamani ya maisha inajitokeza wakati Yohana anapoelezea maneno, 'Uzima wa Milele.' Uzima wa milele ni kiwango cha milele na wingi wa uhai. Uzima wa milele ni wingi wa dhamana ya maisha ambayo yaanzia katika maisha haya, na kuendelea milele.

Yohana anatuambia kwamba hatuna ujuzi wa thamani hii ya uzima wa milele kwa sababu ya tukio letu la kuzaliwa katika mwili. Lakini ikiwa tutapokea ushuhuda huu wa kuzaliwa tena, ambako anakuita 'kuzaliwa kutoka juu', na kwa sababu ya tukio hilo, tutaishi katika hali ya thamani na kiwango cha juu. Tutakuwa na 'uzima tele,' au 'uzima wa milele.'

Katika sura baada ya nyingine, Yohana hatatuambia tu, bali atatuonyesha kile alichomaanisha wakati anapotaja uzima wa milele. Hivyo basi, tunapozidi kusoma kila sura ya Injili hii, twahitajika kuuliza swali hili, 'uzima wa milele ni nini katika sura hii, ndugu Yohana? Unaposoma kila sura, kwa njia ya maombi uliza hivi: 'Katika sura hii ndugu Yohana, Yesu ni nani,? Imani ni nini? Na Uzima ndiyo nini?' Tambua kwamba Yohana atajibu maswali haya kwa uzito mwingi katika kila sura ya Injili hii.

Ufunguo Wa Tano

Ufunguo huu ni ile lugha ya ishara yenye kuvutia ambayo Yohana anatumia katika kuandika. Injili hii ya Yohana imeandikwa katika viwango viwili. Mtoto mchanga anaweza kuelewa kile kiwango cha kwanza. Unaweza kutumia Injili hii hili kuwafundisha watoto wako kusoma, kwa sababu Yohana anatumia maneno mepesi na mengi kuliko waandishi wale wengine wa Injili. Mtoto anaweza kusoma na kufahamu Injili ya Yohana katika kiwango cha kwanza. Hata hivyo, kuna kiwango kingine cha juu chenye maana kuu katika Injili hii. Na mchungaji mkuu mwenye kukomaa kiroho wa Mungu hawezi kufikia kimo hiki cha pili katika Injili hii.

Injili ya Yohana ndiyo niipendayo sana kwa sababu ya kiwango hiki cha pili ambacho Yohana anaiandika hii lugha ya ishara yenye mafumbo, na ya kiroho. Nimefahamishwa kwamba hili kufahamu kitabu hiki cha Injili ya Yohana, tunahitaji shahada au cheti cha elimu ya juu cha *Masters* katika thiolojia na falsafa hili tuweze kufikia kile kiwango cha pili cha Injili. Sikubaliani na maoni hayo. Naamini kwamba twahitaji Roho Mtakatifu kutuonyesha maana ya kiwango hicho cha pili tunaposoma Injili ya Yohana. Unaposoma Injili hii, mwulize Roho Mtakatifu akuonyeshe maana ya kile kiwango cha pili katika kila sura.

Ufunguo Wa Sita

Kuna mtazamo mwingine ambao ningetaka kushiriki nawe tunaposoma hii Injili ya Yohana pamoja. Katika sura ya kumi na mbili, baadhi ya Wayunani walimwendea Filipo kwa ombi hili: *'Bwana, sisi twataka kumwona Yesu.'* Fanya maombi hayo ya Wayunani kuwa yako mwenyewe na ya kibinafsi katika ibada yako ya faraghani unaposoma Injili hii. Ufunguo wangu wa mwisho ambao unafungua lugha hii ya ishara ya Yohana ni kukupa changa moto kusoma Injili hii yote kwa hali ya maombi, ukimwomba Mungu hivi: 'Baba, mimi ninataka kumwona Yesu.'

Ukitenda hivi, utagundua kwamba Injili ya Yohana ni kama 'jumba la kiroho la maonyesho.' Kila sura ni kama 'chumba' katika jumba la maonyesho ya sanaa. Kwenye 'kuta' (mistari au vifungu) katika kila chumba (sura), utapata 'michoro' yenye kuvutia ya Yesu Kristo. Mtume huyu wa upendo anaonyesha 'michoro' hii iliyovuviwa ya Yesu Kristo katika kila sura ya Injili.

Nilipata michoro kumi na tano ya Kristo katika sura ya kwanza na kumi na tano katika sura ya nne. Hebu tazama michoro ni mingapi ambayo unaweza kupata unaposoma Injili hii ya Yohana. Kisha chagua mchoro mmoja wa Yesu katika kila sura ya Injili hii ya Yohana. Hebu fikiria kuhusu kibandiko cha shaba kikiwa chini ya kila mchoro. Hebu kariri kila kibandiko cha michoro hiyo. Kisha nenda usingizini usiku hali upo katika hali ya kuabudu kupitia Injili hiyo ya Yohana, huku ukitafakari juu ya michoro ya Kristo ambayo umeichagua katika kila sura ya Injili.

Hivi ndivyo 'vibandiko vya shaba' vilivyo chini ya michoro yangu, ya Kristo katika kila sura: katika sura ya kwanza hadi ya saba; Mwana kondoo wa Mungu - ambaye anaweza kubadilisha maji yako kuwa divai - Mwokozi wa pekee wa Mungu - Maji ya Uzima - Ufunguo kwa Maandiko - Mkate wa Uzima - Mwalimu kutoka kwa Mungu.

Katika sura ya nane hadi ya kumi na nne; Mwana ambaye hutufanya kuwa huru kabisa - Nuru ya Ulimwengu - Mchungaji Mkuu wa kondoo - Ufufuo na Uzima - Kikoko cha Mbegu ya Ngano ambayo huanguka katika ardhi na kufa hili kumtukuza Baba yake - Mtumishi ambaye alikichukuwa kipanguzo, - Njia na Kweli na Uzima.'

Katika sura ya kumi na tano hadi ya ishirini na moja; Mzabibu unaotafuta Matawi - Aliyemtuma Roho Mtakatifu - Kuhani Mkuu anayeomba – Shahidi wa Kweli - Kristo aliyesulubiwa - Kristo Aliyefufuka na Kristo ambaye Huwajibisha kwa Mwito Mkuu.

Hii ndio michoro ya Kristo inayovutia katika sura hizi ishirini na moja za Injili ya Yohana. Unaposoma Injili hii ya Yohana, nakili kwenye daftari yako michoro ambayo utaipata katika kila sura, iwe ni michoro yako kibinafsi ya Kristo; ambayo itakuwa na maana kuu kwako kuliko michoro yangu, inaweza kugusa maisha yako.

Wazee katika Kanisa nililosimamia hapo mwanzoni waliweka ombi la wale Wayunani katika kibandiko kidogo cha kijisahani cha shaba na kujengewa kwa saruji katika mimbara, hili kila Jumapili wakati mchungaji anaposimama kwenye mimbara, aweze kuona maneno haya: *'Bwana, tungependa kumwona Yesu.'* Wao hawakutaka mchungaji kuona maneno hayo wakati nilipokuwa akihubiri tu, lakini hata wakati walipokuwa na wahubiri wageni. Wazee hawa walikuwa wakisema hivi, *'Sisi twataka kumwona Yesu kila mara Neno la Mungu linapohubiriwa katika mimbara hii.'*

Muombe Roho Mtakatifu akupatie ufunuo zaidi wa Yesu Kristo wakati unaposoma Injili ya Yohana. Kisha jibu maswali hayo mawili: ‘Imani ni nini, na Uzima wa Milele ni nini?’ Wakati unapomwona Yesu, mwamini na uzaliwe mara ya pili, kisha pokea uzima wa milele!

Sura Ya Nane

‘Jumuiko La Injili Ya Yohana’

Wakati wahubiri wanapojifundisha jinsi ya kuhubiri, wao huambiwa mambo matatu. ‘Jambo la Kwanza, waambie kile unataka kuwafunza. Kisha, waambie. Halafu, waambie kile umewafunza!’ Wakati Yohana anapoandika Injili hii yake, misitari yake ya kwanza kumi na minane inafahamika kama utangulizi ambapo yeye atuambia kile anachonuia kutufunza. Kisha kutoka msitari wa kumi na tisa wa sura ya kwanza hadi msitari wa ishirini na tisa katika sura ya ishirini, anatufunza hayo. Mwishowe, katika msitari wa thelathini na thelathini na moja wa sura hiyo aliyofunza, anatukumbusha kile ametufunza.

Wakati anapotuambia kile anachonuia kutufunza, miongoni mwa kweli nyingine, anatuambia wakati Neno linaloishi la Mungu lilifanyika mwili na kuishi kati yetu, wakati walipompokea (kuamini Yeye), au kumpokea Yeye vyema; wao walizaliwa mara ya pili. Walipata ujuzi wa kuzaliwa huko kwa pili ambako hakukuwa ni katika mwili au hali ya kawaida. Wao walizaliwa na Mungu.

Baada ya kutujulisha au kutueleza kile ambacho alikuwa atatufunza, atatupatia mifano ya kile ambacho ameandika kuwa wale waliompokea vyema Yesu walizaliwa kutoka juu. Katika sura moja hadi nyingine, atatupatia mfano wa jinsi watu huzaliwa mara ya pili wakati wanapomkea Yesu Kristo kwa njia njema. Yeye anaanza kwa kutuambia jinsi baadhi ya mitume wa Yesu walivyomjia na kukutana kwa mara ya kwanza na Bwana na Mwokozi wao. Wao walimwuliza mahali ambapo alikuwa akiishi. Aliwakaribisha kwenda kuona alipokuwa akiishi na jinsi alivyokuwa akiishi. Na kwa sababu uamuzi wao kuja kuona, hii iliwaongoza kuishi na kufa kwa ajili Yake. Ni dhahiri kwamba walipata ujuzi wa maana ya kuzaliwa na Mungu wakati walipoishi na Yesu.

Katika sura ya pili, kuzaliwa kwa pili kunadhihirishwa kwa njia ya mafumbo wakati Yesu anapoelezwa kuwa ndiye yule ambaye anaweza kubadilisha maji yetu kuwa divai. Hatua ambazo zinatuongoza katika muijiza huu, na kwa njia ya utekelezaji, katika uzao mpya, ziko katika njia ya mafumbo kwetu. Kwanza, ni katika maneno ya Mariamu: *'Hawana divai* (2:3).**'** Kwa kuwa divai ni ishara ya furaha katika Maandiko, kwa njia ya utendaji wa ibada ya kibinafsi katika faragha, maneno haya ya Mariamu ni kama kukiri kwamba hatuna furaha, au kwamba hatujazaliwa kwa mara ya pili.

Maji wakati mwingine ni ishara ya Maandiko. Tunasoma pia kwamba Neno la Mungu ni 'mbegu' ambayo huleta uzao mpya, kisha tunaambiwa kuwa imani huja wakati tunapolisikiza Neno. Wengine huona katika ile mitungi mikubwa yamkini lita sabini ambayo imejazwa maji, kama picha ya maisha yetu yakijazwa na Neno la Mungu na kuwa kama hatua ambayo hutuongoza katika uzao mpya (2:7; Waefeso 5:26; 1 Petro 1:23; Warumi 10:17).

Maneno ya Mariamu kwa watumishi yanawakilisha ufunguo wa kufanya Neno la Mungu kuwa nguvu katika maisha yetu: '*Lo lote atakalowaambia, fanyeni (*Yohana 2:5)**.'** Huku ukizidi kujaza mawazo na moyo wako kwa Neno la Mungu, lo lote atakalokuambia, lifanye, wakati wote lifanye. Hatua hizi ambazo hutuongoza katika uzao upya zinaweza kutumiwa kama utaratibu wa ufufuo wa kiroho wa mtu binafsi, wakati unapohitajika.

Wale ambao wana ufahamu mwema wa Injili ya Yohana wanafahamu kwamba sura ya tatu ndipo Yesu anamwambia yule Rabi au Mwalimu mkuu, Nikodemo kwamba ni lazima azaliwe mara ya pili. Ni vyema ikiwa tutambua kwamba katika tukio hili lake pamoja na Nikodemo, ndipo Yesu anatumia matamshi haya katika mahojiano Yake na Mwalimu mkuu katika Israeli. Ingawa Yesu halitumii tamshi hili la 'kuzaliwa mara ya pili' na watu wengine, kulingana na Yohana, hivi ndivyo ilivyo kwa wale ambao humpokea Yesu vyema.

Nikodemu anamthibitisha Yesu kwa kumtangaza kuwa Mwalimu, ambaye alitoka kwa Mungu. Mtu fulani alisema hivi, 'Kile ambacho tunaamini kabisa, tunakitenda. Mengine ni maneno matupu ya dini.' Ni kana kwamba mahojiano haya yanaanza naye Nikodemo akimwambia Yesu, 'Mimi nimekiona kile ambacho wewe unakitenda hivyo basi, nimekuja hili kusikiliza mazungumzo yako ya dini.' Baada ya kupokea uthibitisho huo, Bwana anamwambia huyu Rabi kuwa, *'Ni lazima tena. Ni lazima uanze njia nyingine, ni lazima uanze pamoja nami.'*

Yesu anamwambia mwalimu huyu mkuu katika Israeli, kwamba hapaswi kushangaa kwamba anapaswa kuzaliwa mara ya pili, kana kwamba ni vigumu, na isivyoeleweka, au sio lazima. Kulingana na Yesu, kusudi la kuzaliwa upya ni ili upate kuona na kuingia katika Ufalme wa Mungu. Haya ni mafunzo ambayo kwa hakika, yanamsema Mungu kuwa ndiye Mfalme ilhali sisi tu raia Wake. Huu ndio mkazo ambao tumeuona kote katika Biblia ambao umejumuishwa kwa maneno haya: 'Mungu Kwanza!'

Katika mazungumzo haya pamoja na Nikodemo, Yesu anatangaza kuhusu kauli ya mwenyewe kujifikiria binafsi. Anatangaza kwamba ndiye Mwana wa pekee wa Mungu, jibu la pekee kwa shida ya dhambi na Mwokozi wa pekee wa Mungu. Pia asema kwamba katika kumwamini Yeye, wakati anapodai kujihusu mwenyewe kunamaanisha uzima wa milele, na kutokumwamini kunamaanisha hukumu (3:14-21).

Madai haya ya kujifikiria yalifanywa hili kujibu swali la Nikodemo alilouliza mara mbili. Swali hilo lilikuwa ni 'Jinsi gani?' Kwa neno moja, jibu la Yesu lilikuwa 'Amini.' Sehemu yetu katika ujuzi huu wa uzao mpya ni kuamini. Sehemu ya Mungu ni kama upepo. Hatuwezi kuona wala kutabiri upepo. 'Hivi ndivyo alivyo kila mtu aliyezaliwa kwa Roho,' kulingana na Yesu. Ingawa hatuoni kule kuikiri imani kutoka kwa Nikodemo katika mahojiano haya, nakala nyingine kumhusu katika Injili hii, na katika desturi, zinatushawishi kwamba alizaliwa mara ya pili hapo baadaye (7:50; 19:38-42).

Sura ya nne inatuelza hadithi ya mtu wa kawaida, mwenye dhambi na, mwanamke msamaria ambaye alizaliwa mara ya pili. Ingawa Yesu hatumii maneno hayo kwa Msamaria huyo, anatumia mafumbo yake kulingana na mahitaji ya huyu mwanamke. Tunatambua kwamba huu ni mfano mwingine wa mtu ambaye alizaliwa mara ya pili kwa sababu alimpokea vyema Yesu. Anajionyesha kama Maji yaliyo Hai na kumwambia kwamba ye yote anywaye hayo Maji ya Uzima hataona kiu tena.

Anaambiwa kwamba kunywa kwa Maji ya Uzima, kutafanyika ndani yake kijito ambacho wengi watakuja kunywa maji. Haya yanatimizwa wakati anapozaliwa mara ya pili na kuwafikia wanaume wa Samaria kwa ajili ya Kristo. Alivumbua aina mbili ya ujuzi mkuu katika maisha: Kuzaliwa mara ya pili mwenyewe, na kufanyika chombo ambacho kupitia kwake, wengine wanazaliwa mara ya pili.

Hebu tilia maanani maswali yale matatu katika sura nne katika Injili hii. Yesu ni nani? Yeye ndiye Neno la Uzima la Mungu ambaye alifanyika kuwa mwili na kuishi kati yetu hili tuzaliwe mara ya pili. Ndiye anayeweza kubadilisha maji kuwa divai. Ndiye tumaini letu la pekee la Mwokozi. Yeye ndiye Maji ya Uzima ambayo yanakata kiu milele, na kufanyika ndani yetu kijito ambacho wengi huweza kunywea na kuzaliwa mara ya pili.

Imani ni nini? Imani ni kupokea vyema matamshi ya Yesu kuhusu Yeye ni nani. Imani ni 'Njoo uone pale na jinsi anavyoishi maisha Yake.' Imani ni kusikia na kutii Neno la Mungu. Imani ni rahisi kama kuchukua kikombe cha maji ambayo unaamini kuwa yatakata kiu chako.

Na Je! Maisha ni nini? Maisha ni kuzaliwa kwa mara ya pili. Maisha ni kubadilishwa kwa maji yako kuwa divai. Maisha ni kuona na kuingia katika ufalme wa milele wa Mungu. Maisha ni kinywaji cha Maji ya Uzima ambayo hukata kiu milele, na kufanyika ndani yako kijito ambacho wengi hunywea kwa kiu cha ndani, na kiroho katika maisha yao.

Madai Ya Kristo

Sura zifuatazo nne za Injili hii zinanukuu mahojiano marefu, yenye ubishi kati ya Yesu na viongozi wa kidini. Mahojiano haya yanakatizwa wakati mwingine na pia kubadilisha makao na kuzidi kuendelea hadi wakati baadhi ya hawa viongozi waaminifu na wengine wajaribu kumpiga kwa mawe kwa kufuru - kwa kuwa alidai kwamba Yeye ni sawa na Mungu na kwa hakika ni Mungu. Ni wazi kwamba Yesu anataka ubishi huu kutokea. Alithibitisha kusikizwa na hawa viongozi wa kidini kwa kuivunja sheria ya Sabato kwa kusudia.

Alimponya mtu siku ya Sabato kwenye birika ya Bethsaida, ambapo ni hatua chache tu karibu na Hekalu. Alimwamuru mtu huyo kuchukua matandiko yake na kuyabeba mbele ya Hekalu. Ilikuwa kinyume cha sheria ya Sabato. Uponyaji huu ulikuwa chanzo cha mahojiano yenye uhasama ambayo yaliendelea kote katika sura ya nane.

Uponyaji wa mtu huyu unaendeleza mfano wa Yohana kuhusu watu ambao walizaliwa mara ya pili wakati walipompokea vyema Yesu. Katika tukio hili, kuna watu wengi wagonjwa na Yesu amponya tu mtu mmoja wao. Inawezekana kwamba alimponya mtu huyu kwa kuwa labda alikuwa amekata tamaa kuhusu birika ile ya maji, na cho chote chenye imani ya ushirikina kuhusu uwezo wa uponyaji wa birika hiyo. Katika hadithi hii, imani inafanyika kuwa kukata tamaa juu ya mambo yote ambayo hayawezi kutufanya kuwa wazima.

Wakati mazungumzo yanapoanza, Yesu anaanza kwa kufanya madai ambayo yanamfanya kuwa asiye wa kawaida: Anadai kwamba Mungu ameweka hukumu yote juu Yake. Anadai kwa ujasiri mwingi kwamba Yeye anaweza kufanya yale yote ambayo Mungu anaweza kufanya. Ikiwa tunaweza kupata daftari na kuandika madai haya yote ya Yesu, basi tutaona kwamba atatuachia baadhi ya maamuzi katika Yeye au kumpiga kwa mawe na kumtoa nje ya maisha yetu milele. Kwa maneno yake mwandishi mmoja wa Uingereza, 'yamkini kwamba tumwite mwongo, au tuwe wenye huruma na kumtaja kama kama mwenye kichaa, au tumwite Bwana wetu, kisha tumwabudu na kumfuata.'

Baada ya kufanya madai hayo ya kushangaza, Yesu aliwaambia viongozi wa dini kwamba wao hawajakosa thibitisho la kaamini madai yake. Wao walimheshimu Musa, hivyo basi Yesu alidai kwamba Musa aliandika mambo kuhusu Yeye. Wao hawangepinga hoja kwamba Yohana Mbatizaji alikuwa nabii. Hivyo basi, Yesu ananukuu maneno ya uthibitisho ambayo Yohana aliyazungumza kuhusu Bwana wake. Ananukuu maneno ya Mungu Baba katika ubatizo wake kama ushahidi wa kweli wa madai yake. Pia atupatia misitari yenye ufunguo katika Biblia nzima wakati anawaambia wamba Maandiko yamshuhudia Yeye na kuthibitisha ukweli wa madai yake (5:39, 40).

Katika sura ya sita, Yeye anafuatilia muijiza wa kuwalisha wale watu elfu tano kwa hoja yenye uzito mwingi iliyo ngumu. Mahojiano yake kuhusu Mkate wa Uzima kwa hakika ni kuhusu kazi yenye maana. Yeye anaanza sehemu hiyo ya mahojiano kwa kuwaambia wale viongozi wa dini kwamba wao walikuwa wakitenda kazi isiyo na maana. Walipomwuliza kile ambacho Yeye hutenda mchana kutwa, aliwaambia kuhusu kazi Yake.

Anadai kwamba huwa ananena maneno ambayo ni Roho na Uzima, ambayo Mungu humwambia. Wakati watu wanapopokea vyema maneno hayo, wao huvumbua kwamba Yeye ndiye Mkate wa Uzima ambao umeshuka chini kutoka mbinguni. Katika sura ya nne, Yeye ndiye Maji ya Uzima. Katika sura hii, Yeye ndiye Mkate wa Uzima.

Wengi wa wanafunzi waliacha kumfuata baada ya mahojiano haya kwa sababu alisema kwamba ni 'Lazima wao wale mwili wake na kunywa damu yake' hili wawe na uzima wa milele kulingana na madai yake kuhusu Mkate wa Uzima. Kwa hali hii, Petro anatupa jibu nzuri kwa swali hili: 'Imani ni nini?' Wakati Yesu anapomwuliza Petro kama atamkana na

kumwacha, kwa maneno mengine, Petro anasema hivyo, ingawa haelewei. Kama alivyo Petro, ni lazima tuamini na kumfuata Yesu hata wakati hatuelewi.

Yesu alikuwa kwa hakika akifundisha kwamba kunywa na kula ni mfano wa imani. Wewe unaamini kwamba kikombe cha maji kitakata kiu na kukoa maisha yako. Unadhihirisha imani yako wakati unapochukua kikombe cha maji na kunywa. Unaamini kwamba ule mkate utakuondolea njaa, hivyo basi unakula. Imani ni kunywa na kula, kulingana na Yesu.

Kula mwili wake kulimaanisha kuamini yale yote ambayo alifundisha na kuyaonyesha kwa mfano wakati Neno la milele lilipofanyika kuwa mwili. Kunywa damu yake kunamaanisha kuamini maana ya kifo chake msalabani - kwamba Yeye alikuwa Mwana kondoo wa Mungu wakati alipofariki. Kwa upande mwingine wa Meza ya Bwana na msalaba ambao maanake, ni rahisi kufahamu hii fumbo ngumu. Mitume pamoja na wanafunzi hawakuwa na fursa ya mtazamo huu.

Katika sura ya saba, dai lake ni kwamba mafundisho yake ni mafundisho ya Mungu. Wakati hilo dai linapohojiwa, Yeye atupatia jibu lingine jema kwa swali kuhusu imani. Anawaambia kwamba wale ambao wanakaribia mafunzo yake wakiwa na hamu ya kutenda yale yanayofundishwa, watafahamu kwamba mafundisho yake ni ya Mungu (7:17). Mwito wa wenye maarifa wa ulimwengu ni ‘wakati ninapofahamu, basi nitatenda.’ Kule kufahamu huongoza katika kutenda. Kulingana na Yesu, kufahamu huongoza kutenda.

Sura ya nane huleta majadiliano kwa kumalizia kwenye nguvu. Yesu anahubiri kwa uwezo mkuu anapowaambia hawa viongozi wa dini kwamba wao ni wana wa Ibilisi na wamo katika utumwa wa baba yao muovu. Yeye anawaambia kuwa ni watumwa wa dhambi na kwamba watakufa katika dhambi yao ikiwa hawataamini. Anadai kwamba alitoka mbinguni, ilhali wao wanatoka Jehanamu, na kwamba wanaelekea huko ikiwa hawataamini.

Anapomaliza huu ujumbe wa ajabu, wengi miongoni mwa hawa viongozi wa dini wanaamini (8:30-36). Wakati anapopokea maungamo ya imani yao, anatoa sehemu tatu za uzao mpya.

Hatua ya kwanza kuelekea uzao upya ni kuamini. Anawaambia wale ambao hukiri kuamini katika Yeye waendelee katika Neno lake na wafanyike wanafunzi wake kwa hakika.

Anafafanua kwamba sehemu ya pili ni kuendelea katika Neno lake na kufanyika wanafunzi wake.

Anazidi kuelezea sehemu ya tatu wakati ambapo anahidi kwamba watakuwa na ujuzi ambao utawafanya kuwa huru kweli. Sehemu ya tatu ni kwamba kuendelea katika Neno lake kutawaongoza kujua, kupitia ule uhusiano kwamba Yeye ndiye Kweli. Ahadi yake ni kwamba wakati Mwana anapowaweka huru, wao watakuwa huru kweli. Sehemu ya tatu ya uzao upya itakuwa ni kama kutoka gerezani, kulingana na ahadi ya Yesu (8:30-36).

Madai yake ya mwisho katika mahojiano haya ni wakati wale Wayahudi ambao hawaamini, wanapomshtaki kwa kusema kwamba anamfahamu Ibrahimu. Yeye aliwajibu, *'Kabla yake Ibrahimu, Mimi nipo!'* Hapo ndipo wengine kati yao walipojaribu kumpiga kwa mawe. Hebu tilia maanani madai haya yote ya Yesu, kisha kwa njia ya maombi, jibu swali hili ambalo Yesu aliwauliza mitume Wake*, 'Nanyi mwaninena mimi kuwa ni nani?* (Mathayo 16:15).'

Sura ya tisa inaanza kwa muijiza wa uponyaji ambao ulifuatiwa na hoja lingine kutoka kwa Yesu. Wahubiri wa siku ya leo huileta kweli ambayo wanataka kuihubiri kisha kuidhihirisha. Kama manabii Yeremia na Ezekieli, walianza mahubiri yao kwa ishara zenye mafumbo, au kwa mfano wenye kuigiza ambao uliwavutia wasikilizaji wake. Yesu anaanza mazungumzo yake kuhusu Yeye kuwa Maji ya Uzima, Mkate wa Uzima, pamoja na Nuru ya Ulimwengu, na matokeo yaliyotangulia ujumbe huo kabla ya mahubiri.

Baada ya kumfanya kuona mtu mwenye umri wa miaka arobaini, ambaye alizaliwa akiwa kipofu, Yesu alihubiri kwamba Yeye alikuwa Nuru ya Ulimwengu. Alidai kwamba alikuwa Nuru ambayo ilidhihirisha upofu wa wale ambao walikuwa wakikiri kwamba wanaona, na kuwafanya kuona wale ambao walifahamu kwamba wao ni vipofu.

Wachimba migodi ya makaa walikuwa wamenaswa kwa siku tatu mchana na usiku kutokana na mlipuko ambao ulisababisha maporomoko katika migodi hiyo. Walipata kuokolewa hapo mwisho. Wakati mmoja wa wachimbaji alipowauliza wale waliowaokoa ni kwa sababu gani hawakuwa na taa, wale wachimbaji pamoja na waokoaji walitambua kwamba yule mchimbaji alikuwa amepofushwa na ule mlipuko. Alifanyika kipofu kwa siku tatu, ingawa hakutambua hivyo hadi wakati waokoaji hao walipokuja ambao walikuwa na taa nyingi. Yesu

alikuwa akidai kwamba Yeye alikuwa Nuru ya aina hiyo - Nuru ya ulimwengu ambayo huwapa mwanga wale ambao ni vipofu wa kiroho, na kudhihirisha upofu wa wale ambao hawafahamu kwamba wao ni vipofu.

Wakati viongozi wa kidini walipotambua kile alichokuwa akikinena, walimwuliza ikiwa alikuwa akiwaambia wao kwamba ni vipofu wa kiroho. Yeye aliwajibu kwa kuwaambia kuwa kama wangekuwa vipofu, basi wasingekuwa na dhambi. Lakini kwa sababu walijivunia kweli kwamba walikuwa wakiona, basi hawakuwa na sababu ya dhambi yao. Uamuzi wa kithiolojia ni, kuwa na nuru, huna dhambi, na kiini hasa cha dhambi ni kukataa nuru, kulingana na Yesu (9:40, 41; 15:22).

Sura ya kumi ni kama mfululizo wa zaburi ya mchungaji ya Daudi. Yesu kwa ujasiri, anadai kuwa Mchungaji Mwema ambaye Daudi aliandika katika zaburi ile. Mafumbo ambayo anatumia yanatangaza kwamba Yeye anawaongoza Wayahudi wanao mcha Mungu kutoka katika dini yao iliyothibitishwa hili kumfuata katika wokovu. Hii ina matumizi ya hakika kwa yule kipofu ambaye aliponywa, na kufukuzwa kutoka Sinagogi kwa kuwa alikiri Yesu kuwa Bwana wake.

Sura ya kumi na moja ni ya ufufuo katika Injili hii. Hadithi hii yenye kuvutia inaonyesha jinsi Yesu anavyoruhusu watu watatu kushuhudia shida mbili za kimaisha ambazo hazijawahi kuwa na jawabu - Ugonjwa na Kifo. Hii ni kwa sababu Yeye anawapenda. Alitaka wao kujifunza kwamba Yeye ndiye Ufufuo (ushindi juu ya mauti), na ufunguo wa uzima wa milele. Wao walijifunza kupitia kifo cha Lazaro kwamba yule ambaye anaamini na kuishi katika umoja na Kristo hatakufa kamwe (11:25, 26). Hadithi hii ya kimiujiza imewaletea mamilioni ya watu uvuvio pamoja na uzima wa milele katika karne zote za historia ya Kanisa.

Sura ya kumi na mbili inagawa Injili ya Yohana katika sehemu mbili. Karibu nusu ya sura zilizopo katika Injili hii zinagusia miaka thelathini na mitatu ya kwanza ya maisha yake Kristo, na nusu ile nyingine yagusia juma la mwisho la maisha Yake. Kote katika Injili hii, tunasoma fungu hili la maneno, *'Wakati wake haukuwa umefika.'* Katika sura hii tunamsikia Yesu akiomba hivi, *'Baba, wakati umewadia. Ni kipi ambacho nitakinena? Nikomboe kutoka wakati huu? Lakini ni kwa wakati huu nilikuja ulimwenguni. Baba litukuze jina Lako.'* Nayo sauti ikanena kutoka juu mbinguni na kusema, '*Nimelitukuza Jina langu hapo mwanzoni kupitia maisha Yako, nami nitalitukuza tena.'*

Yesu aajitenga na kwenda Orofani na wale kumi na wawili. Anfanya mkutano ambao ninautaja kuwa wa mwisho wa Kristo. Alianza huduma yake kwa mkutano wa faragha wa kwanza wa Wakristo' alipokuwa akihubiri juu ya mlimani. Hapo ndipo alipowachagua mitume hawa. Yeye amewafundisha na kuwaonyesha pamoja na kuwafunza kwa matendo kwa muda wa miaka mitatu. Mkutano wa mwisho wa faragha ndio 'kuhitimu' kwao kutoka kwa mafunzo yao ya miaka mitatu katika 'seminari.'

Na katika hali hii, anatoa majadiliano yaliyo marefu zaidi kuwahi kunakiliwa ambayo yanaitwa, 'Mazungumzo ya Orofani.' Yamenakiliwa katika sura ya kumi na tatu hadi kumi na sita ya Injili hii. Wengine huongeza sura ya kumi na saba ambapo Yesu anawaombea mitume maombi yaliyo makuu, pamoja na wale ambao watakuja kuamini kupitia hao ambao ni wewe na mimi.

Mazungumzo haya kwa hakika ni mjadala wa faragha kati ya watu walio na urafiki wa karibu sana. Wao wanamwuliza maswali, na mengi ya majadiliano haya ni majibu kwa maswali yao. Katika sura ya kumi na tatu, tunasoma kwamba alianza majadiliano haya kwa kitendo cha fumbo cha kuwaosha miguu. Luka anatuambia kwamba katika safari yao kwenda katika orofani, walikuwa wakibishana kuhusu ni nani angekuwa mkuu katika ufalme ambao walikuwa wakidhania kwamba Yeye ataimarisha (Luka 22:24-30). Ni lazima kuwa jambo hili liliwasumbua sana wakati Bwana alipoamua kuwaosha miguu yao wote.

Alipomaliza kuosha miguu yao, aliwauliza hivi, *'Je! Mwafahamu ni nini niliyowatendea?* (12).' Swali hilo linajibiwa katika msitari wa kwanza katika sura ile ambayo tulisoma haya, '*Baada ya kuwapenda wale waliokuwa ni wake waliokuwepo humu ulimwenguni, Yeye aliwaonyesha wao kiwango chote cha upendo wake.'* Aliwapa matumizi haya, '*Mimi nimewapa ninyi mfano. Ikiwa mimi nimewaosha miguu yenu, ni wajibu wenu pia kuoshana miguu yenu.'*

Baadaye, alijibu swali hili na kuonyesha kwa njia yenye uwezo mkuu wakati anapofunza kuwa: *'Amri mpya nawapa, Mpendane. Kama vile nilivyowapenda ninyi, nanyi mpendane vivyo hivyo. Hivyo watu wote watatambua ya kuwa ninyi mmekuwa wanafunzi wangu, mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi* (13:34,35).'

Alikuwa amewapenda kwa muda wa miaka mitatu kwa njia ambazo wao hawakuwa wamezifahamu hapo mwanzoni. Wote walikuwa katika chumba cha orofani kwa kuwa Yeye alikuwa amewapenda na walikuwa wamefanya bidii kurejesha upendo huo. Walikuwa wamefanya maagano na kujitolea kwake Kristo walipokuwa wakikutana naye kwa mara ya mwisho kabla ya kifo chake. Amri hii mpya aliyowapa ni changa moto kufanya agano na kujitolea upya - kujitolea mmoja kwa mwingine. Kwa amri hii mpya, aliunda jamii mpya ambayo ingefanyika kuwa Kanisa lake. Alitaka jamii hii mpya kuwa ya watu ambao wamependana.

Katika sura ya kumi na nne, alihubiri 'Ujumbe wa Mazishi' kabla ya kifo chake. Aliwaambia kwamba alikuwa akiwaondokea (maana kwamba alikuwa akienda kufa), lakini mioyo yao isifadhaike kwa sababu kuna mahali ambapo anatayarisha kwa ajili yao. Mioyo yao isifadhaike kwa sababu kuna mtu ambaye atawafariji. Kwa sababu ya mfariji huyo, kila mara watakuwa na amani isiyo ya kawaida mioyoni mwao ambayo anawaambia kuwa ni 'Amani Yangu.'

Tena aliwafariji kwa kuwaambia kuwa uhusiano baina yao utakuwa wa karibu baada ya kifo chake. Yeye aliwaambia kuwa ufunguo wa uhusiano huo utakuwa ni utiifu wao kwake na kwa Maandiko Yake ambayo Roho Mtakatifu atayabariki kwa kuwezesha kufanya ukaribu naye Mwokozi. Ufunguo wa maneno na kazi Zake ulikuwa ndio ukaribu Wake na Mungu Baba, ilhali ufunguo wa maneno na kazi zao utakuwa wa ukaribu wao Naye kupitia Mfariji, Roho Mtakatifu (10:30; 14: 22,23).

Baada ya kufunza mambo hayo katika chumba cha Orofani, aliwaongoza hadi katika bustani na kuwapa hotuba ya kuadhimisha kuanza kazi kwao. Aliushusha mzabibu wenye matawi mengi yaliyokuwa na matunda. Kisha akatoa mfano kwa kile ambacho tayari alikuwa amewafunza katika chumba cha Orofani na kwa fumbo lenye uzito sana. Baada ya kuwaelekeza kwa kweli kwamba yale matunda yalikuwa yamezaliwa kwa sababu yale matawi yalikuwa yameunganishwa kwa mzabibu, Aliwahimiza kukaa pamoja na kuwa ndani Yake, pamoja na kuwahahidi kwamba wangezaa matunda mengi ikiwa wangetenda hivyo.

Tena aliwapa sababu sita kwa nini ilikuwa ni lazima wazae matunda. Ni lazima wangezaa matunda kwa sababu hii ni njia moja ambayo wangeonyesha ulimwengu kwamba wao walikuwa mitume Wake. Ni lazima wazae matunda kwa sababu hii ilikuwa ndio njia ambayo wangemtukuza Mungu, na ingewaletea furaha kuu. Pia aliwachagua na kuwafanya

kuzaa matunda ambayo aliwaamuru na ni lazima na kwa sababu hana njia nyingine ya kufika ulimwenguni ila tu kupitia wao (15:1-16).

Shairi limeandikwa ambalo linamwonyesha Yesu juu ya wingu baada ya kifo na ufufuo Wake. Yeye anajadiliana kuhusu maisha pamoja na kazi Yake na Malaika, pamoja na mpango Wake wa kuufikia ulimwengu kupitia mitume. Mmoja wa Malaika anauliza ni kitu gani atakachotenda ikiwa mitume hawataufikia ulimwengu kwa ajili Yake? Jibu lake kuwa, *'Basi mimi sina mpango mwingine!'*

Sababu ya mwisho kuhusu mitume kuzaa matunda ni kwamba, Yeye ndiye mzabibu nao ni matawi ya kipekee aliyo nayo. Fumbo hili ni himizo kwao hili wapate kuzaa matunda, hotuba yake ya kuwatuma kuanza huduma na kumwonyesha Kristo jinsi alivyokuwa hata siku ya leo: Mzabibu unaotafuta matawi.

Katika sura ya kumi na sita, Yeye anawahidi kuwatumia Roho Mtakatifu ambaye anamwita Mfariji. Anaelezea utu na kazi yake katika huduma ya Roho Mtakatifu wakati atakapokuja. Sura hii ilitimizwa siku ya Pentekoste.

Katika sura ya kumi na saba, anaomba maombi yenye uvuvio yaliyo na uzito sana kwa hawa mitume. Kote katika Injili ya Yohana, ananukuu kazi ambayo anahitajiwa kufanya. Unaposoma maombi haya, inakuwa dhahiri kwamba hawa mitume ni mojawapo ya kazi Yake muhimu. Katika theluthi moja ya ombi hili, Yeye anaomba kwa ajili ya kazi Yake na kufanya madai kwamba Yeye amemtukuza Baba kwa kuimaliza kazi ambayo Alimpatia kuitenda.

Kisha anaiombea kazi ya mitume ambao ni rasilmali Yake kwa miaka mitatu ya huduma. Ile theluthi moja ya mwisho ya ombi hili kwa wale ambao wataamini Habari Njema kupitia mitume. Hii inamaanisha kwamba aliombea Kanisa Lake. Aliomba kwamba tuishi kwa njia ya umoja usio wa kawaida pamoja Naye, na pamoja na waaminifu wengine, hili ulimwengu upate kujua na kuamini kwamba Mungu Baba anawapenda vile anavyompenda Mwanawe.

Unapoongeza baadhi ya mistari mingine katika sura ile ya ishirini kwa dhana hii iliopo katika ombi hili, unakuwa na mtazamo wa Yohana wa Mwito Mkuu. (20:21). Kwa sababu hiyo, hawezi kuomba kwamba Mungu awachukue mitume au Kanisa kutoka ulimwengu huu kwa sababu ametutuma ulimwenguni kuwatafuta na kuwaokoa waliopotea (17:18).

Maneno Ya Mwisho

Wasomi wengi wanaamini kwamba Injili ya Yohana inamalizikia katika msitari wa thelathini na moja sura ya ishirini. Sura hiyo ya ishirini na moja imekuwa sehemu ya Injili hii tangu kuandikwa kwake, lakini wasomi wanaamini kwamba ni maneno ya ziada. Katika sura hii ya kumalizia, Yesu anawakumbusha mitume saba kati ya kumi na wawili – akiwepo Petro - kwamba Yeye hakuwapa mwito wa kuvua samaki, bali watu! (21:1-14).

Hawa mitume walikuwa wamejishughulisha na kazi bure usiku kucha katika safari yao ya uvuvi. Toka ufuoni, Yesu aliwaongoza kutupa nyavu zao upande ule mwingine wa mtumbwi wao. Punde tu, wakati samaki walipojaa katika nyavu zao, Yohana alifahamu kwamba yule mgeni kwenye ufuo wa bahari alikuwa Bwana.

Huku ni kutokea kwingine kwa Yesu ambapo hatambulikani na wanafunzi Wake ambao walimfahamu na kumpenda (Luke 24:30,31). Ulikuwa uvuvi wa samaki usio wa kawaida uliowafanya kumjua mgeni kwenye ufuo wa bahari kuwa Bwana wao. Wakati Petro alipotambua kwamba ni Bwana, mara tu alijitumbukiza kwenye maji na kuogelea hadi kwenye ufuo wa bahari. Bwana aliwaandalia kifungua kinywa cha samaki na mkate, ambacho tayari alikuwa ametayarisha.

Yesu anafanya mahojiano ya kuvutia sana na Petro katika hali hii ambayo alikuwa akimfundisha mtu ambaye angekuwa kinara cha Kanisa, masomo matatu yenye umuhimu mkuu kuhusu kuvua watu kama wale tuliowatilia maanani wakati tulipochuguza mahojiano na Petro ambayo yalinukuliwa na Luka (Luka 5:1-11). Tunaweza kusema kwamba katika hoja hili, Yesu alikuwa akimfanya mtu kutoka kwa kitu ambacho hakikuwepo (21:15-17).

Tangu siku ile ambayo walikutana, Yesu alikuwa akimfunza Petro mafunzo matatu: Kwamba yeye hakuwa kitu, na kwamba alikuwa mtu, na kile ambacho Yesu angetenda na mtu ambaye amejifunza kuwa si kitu. Petro alikuwa akijifunza somo la kwanza tangu wakati alipokutana na Yesu hadi wakati alipotoweka gizani, na kulia kwa uchungu mwingi kwa sababu alikuwa amemkana Bwana mara tatu.

Katika hoja hili, Yesu alikuwa akijaribu kumfunza Petro somo la pili: Kwamba yeye alikuwa mtu. Katika siku ya Pentekoste, Petro, Kanisa pamoja na ulimwengu mzima ulijifunza somo la tatu: Kile ambacho Kristo aliyefufuka na anayeishi anachoweza kutenda na mtu ambaye amejifunza kwamba yeye si kitu.

Saba kati ya watu wale waliokuwa pale asubuhi pia walikuwapo katika chumba cha orofani wakati Petro alipokuwa akijivuna kwamba alimpenda Bwana kuliko mtu mwingine miongoni mwao. Mbele ya wale watu saba, Yesu anaingia katika mazungumzo na Petro. Kuna uwezekano wa tafsiri kadhaa kuhusu maana kuu ya maswali na majibu ambayo Yesu na Petro walibadilishana katika mazungumzo hayo. Uwezekano mmoja ni kwamba Yesu anamwuliza Petro ikiwa kwa hakika anampenda zaidi ya hawa wengine ambao waliungana nao kwa kifungua kinywa ufuoni mwa bahari.

Tafsiri nyingine ni kwamba Yesu amwuliza Petro ikiwa yeye anampenda zaidi ya wale samaki aliokuwa amewavua siku hiyo. Hii ni pamoja na biashara yenyewe ya kuvua samaki. Jinsi tulivyojifunza katika mazungumzo yaliyopita ya Petro na Bwanake, Yesu alikuwa amemwamuru ‘kuvua watu’ na sasa alikuwa amerudi kuvua samaki (Luka 5:1-11).

Hili kuelewa vema mahojiano baina ya Yesu na Petro, na kuona juhudi waliokuwa nayo katika kusemezana, ni muhimu kufahamu katika lugha ambayo mazungumzo hayo yalinakiliwa kwetui, maana ya maneno ya upendo ambayo yalikuwa yakipitishwa kati yao. Kwa mfano, wakati Yesu alipomwuliza Petro kati ya wale saba, ikiwa upendo wake Kwake ulikuwa mkuu kuliko wao, Yesu alitumia neno la Kiyunani ‘Agape.’

Hii inamaanisha kwamba Yesu alikuwa akimwuliza Petro ikiwa upendo wake ulikuwa mkuu, wa kujitolea kikamilifu bila masharti (1 Wakorintho 13:4-7). Wakati Petro alipojibu kwamba alimpenda Bwana, alitumia neno ‘phileo.’ Umuhimu wa jambo hili ni kwamba, yeye anakiri upendo wake kwa Yesu kuwa ni ule wa juu juu na wa kirafiki tu.

Yesu amwuliza Petro kwa mara ya pili ikiwa kwa kweli anampenda Bwana. Na kwa mara nyingine Yesu alitumia neno ‘Agape.’ Lakini kwa wakati huu, hamwulizi Petro ikiwa upendo wake kwa Bwana ni mkuu kuliko wa wale mitume saba. Petro anajibu tena akitumia neno ‘phileo.’ Petro ananaeleza kwamba upendo wake kwa Yesu ni wa kirafiki tu.

Na kwa mara ya tatu, Yesu anamwuliza Petro ikiwa anampenda Bwana, ila kwa wakati huu, Yesu anatumia neno 'phileo.' Kwa sasa, Yesu anamwuliza Petro ikiwa upendo wake kwa Bwana wafikia kimo cha urafiki. Naye aonekana kwamba amekwazwa na kujibu kuwa, '*Bwana, wewe wayajua mambo yote. Wewe wajua kwamba mimi nakupenda wewe,'* na kwa mara ya tatu, anatumia neno la Kiyunani 'phileo.' Petro alikuwa akimwambia Yesu, 'Wewe wajua, kwamba mimi ni rafiki yako.'

Maneno haya ya Kiyunani yanatuambia kwamba Petro alikuwa amevunjika. Hajivuni wakati huu kama alivyokuwa wakati walipokuwa katika chumba cha orofa. Sasa, anakiri kuwa na ufahamu wa mafunzo hayo mawili kuhusu baraka: Anaomboleza kwa sababu anajifunza kwamba kwa kweli, yeye ni maskini wa roho.

Hoja hii kati ya Yesu na Petro lina uzito mwingi wakati tunapotambua kwamba kila wakati Petro anapokiri upendo wake kwa Bwana kuwa duni, Bwana anamshauri kulisha kondoo wake kulingana na toba yake. Mchungaji Mkuu wa kondoo anatoa matamshi wazi kwamba anataka mtu mwenye ujuzi wa kule kushindwa kuwalisha kondoo na kule kuwafahamu wa kushidwa kwa kondoo Wake. Ni dhahiri kwamba Bwana hataki watu ambao hujidai kuwa wakamilifu ilhali hawana ufahamu, wala utambuzi wa kweli kuhusu kondoo Wake.

Ni kwa sababu gani Kristo aliyefufuka alijidhihirisha kwa nguvu ndani ya Petro siku ya Pentekoste? Wakati tunapofahamu uwezo wa hoja pale ufuoni mwa bahari asubuhi hiyo, tutakuwa na jibu kwa swali hilo. Zaidi ya mitume wale wengine, ni Petro pekee ambaye alikuwa amejifunza kile Kristo angetenda kupitia mtu aliyejifunza kwamba yeye ni duni.

Katika hali hii, Yesu pia anafunza umuhimu mkuu kuhusu mapenzi ya Mungu kwa maisha ya mwanafunzi (21:18-23). Wakati mwingi Petro alikuwa akidai kwamba alikuwa tayari kufa kwa ajili ya Yesu. Katika sura hii ya kumalizia Injili, tunasoma kwamba Yesu aliamua kumwambia Petro jinsi kifo chake kitakavyokuwa. Hii inamaanisha kuwa Yesu alimwambia Petro kwamba alikuwa asulubiwe kichwa chini kwa ajili ya Bwanake.

Wakati Petro anaposikia hayo, bado anadhihirisha utu wake kwa kuelekezea kidole kwenye benga la Yohana, huku akimwuliza Yesu*, 'Je, huyu atakuwa vipi? Mapenzi yako kwa maisha na kifo chake ni yapi?'* Yesu amjibu Petro kwa kumwambia kwamba mapenzi yake

kuhusu maisha na kifo cha Yohana hayamhusu hata kidogo. Neno la Bwana kwa Petro ni hili, *'Ni nini kwako wewe? Nifuate Mimi!'*

Katika hali ya Mungu, tumeumbwa kuwa tofauti na wengine. Sisi hurejeshewa utofauti huo kupitia wokovu. Basi, ni kwa sababu gani tunatarajia kupata mapenzi ya Mungu kwa ajili ya maisha yetu, ambayo yatatufanya kuwa na utofauti huo

Kwa kutokea baada ya ufufuo Wake, ni dhahiri kwamba Yesu anakumbusha mitume wake kwamba wao tayari wameamrishwa kuvua watu. Pia anawahimiza kuchunga na kulisha kondoo waliopotea ambao watafikiwa kupitia mavuno makuu ambayo yaja.

Katika mazungumzo yake na Petro, Yesu anawapa changa moto mitume hili kuvumbua mapenzi Yake kwa maisha yao hasa katika wajibu wa kila mtu ambaye Yeye angependa kutumia katika uvunaji na huduma ambayo itaanza siku ya Pentekoste wakati Kanisa litakapozaliwa.

Sura hii ya mwisho ya Injili ya Yohana ni kama wimbo ulio na sehemu tatu. Sehemu ya kwanza ni changa moto ya Yesu kwa mitume hawa katika kuhusika kwao katika mavuno makuu ambayo yalikuwa yaja. Sehemu ya pili ni changa moto kwa Petro na wale mitume saba kuhusika katika ulezi na uchungaji wa wale wanaouhakika wa kuvunwa. Sehemu ya tatu ni kwa ajili yao wenyewe pamoja nasi katika uvumbuzi wa mapenzi ya Mungu kwa maisha yetu tunapotii mwito Wake mkuu.

Wakati waandishi wa Injili tatu za kwanza wanapotangaza kifo cha Yesu juu ya msalaba, wao wanaeleza kwa ufupi sana kwa kutumia neno: 'wakamsulubisha.' Kwa sababu hiyo, karibu nusu ya sura za za Injili ya Yohana zimewekwa wakfu katika juma la mwisho la maisha Yake, baada ya kufa na kufufuka katika wafu. Injili hii ina nakala kamili ya pingamizi hii kuu katika maisha ya Kristo. Jinsi tayari nimeeleza, nina vitabu vingine sita ambavyo vina maelezo zaidi ya vipindi mia moja kuhusu Injili hii ya Yohana. Nitabakisha katika vitabu hivyo maelezo yangu kuhusu mtazamo wa Yohana juu ya kifo na ufufuo wa Yesu Kristo.

Nitamalizia uchambuzi wa Injili hii ya Yohana kwa changa moto. Baada ya kumaliza kusoma Injili hii yenye uzito, na kutafakari juu ya Kristo pamoja na kujiuliza mwenyewe, Yesu ni nani, na imani ni nini?; kwa hali ya maombi, jiulize mwenyewe ikiwa kwa imani unamfahamu

Yesu Kristo na kama umesoma Injili hii. Ikiwa unamfahamu kwa imani, basi una uzima wa milele kwa sababu, kama ilivyo tawi kwa mzabibu, uko katika ushirika na Kristo aliyefufuka milele.

Mwanafunzi wa Kristo aliye na ushirika wa aina hiyo, alitafakari juu ya hali ya kisasa yenye kumkufuru Kristo na kusema, *'Mimi naamini kwamba Yeye ndiye, ni hao hawana uhakika alikuwa nani. Ingawa pia hawana uhakika kwamba alitenda, mimi nafahamu kwamba angali akitenda.'* Roho nyingine kuu yasema hivi, *'Kristo aliyefufuka ndiye anayedai kuwa.'* Mwingine alisema, *'Kristo aliyefufuka ambaye hudai kuwa ni Yeye, na ana uwezo wa kufanya cho chote ambacho hudai anaweza. Wewe ni yule anayedai kuwa uko, na unauwezo wa kutenda cho chote anachodai unaweza kutenda kwa Yeye ndiye na yuko nawe.'*

Hivi ndivyo Petro alivyojifunza kutoka kwa Bwana akiwa kwenye ufuo wa bahari asubuhi ile. Maombi yangu ya dhati na daima ni kwamba utajifunza thamani za uzima wa milele unaposhuhudia uzima huo kwa sababu umechuguza Injili niipendayo sana.